# القرآن الحكيم

# QURANI TAKATIFU

Swahili Quran Translation

by
Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy
(Former Chief Kadhi of
Zanzibar & Kenya)

29. Na kama mnamtaka Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na nyumba ya akhera, basi Mwenyezi Mungu Amewaandalia wafanyao mema hayo, miongoni mwenu, malipo makubwa.

وَإِن كُنتُنَّ تُرِدْنَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَالدَّارَ الْآخِرَةَ
فَإِنَّ اللَّهَ أَعَدَّ لِلْمُحْسِنَاتِ مِنكُنَّ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٢٩﴾

30 Enyi wake wa Mtume! Atakayefanya maovu dhahiri miongoni mwenu, atazidishiwa adhabu mara mbili; na haya ni sahali kwa Mwenyezi Mungu.

يَا نِسَاءَ النَّبِيِّ مَن يَأْتِ مِنكُنَّ بِفَاحِشَةٍ مُّبَيِّنَةٍ
يُضَاعَفْ لَهَا الْعَذَابُ ضِعْفَيْنِ ۚ وَكَانَ ذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ
يَسِيرًا ﴿٣٠﴾

31. Na miongoni mwenu atakayemtii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na kutenda mema, Tutampa malipo yake mara mbili, na kumwandalia riziki yenye hishima.

وَمَن يَقْنُتْ مِنكُنَّ لِلَّهِ وَرَسُولِهِ وَتَعْمَلْ صَالِحًا
نُّؤْتِهَا أَجْرَهَا مَرَّتَيْنِ وَأَعْتَدْنَا لَهَا رِزْقًا كَرِيمًا ﴿٣١﴾

32. Enyi wake wa Mtume, nyinyi si kama yoyote tu katika wanawake wengine. (Nyinyi wakeze Mtume). Kama mnataka (kufanya jambo la) kumcha Mwenyezi Mungu, basi msilegeze sauti (zenu mnaposema na wanaume) ili asitamani mtu mwenye ugonjwa moyoni mwake (kufanya mabaya na nyiye) na semeni maneno mazuri:

يَا نِسَاءَ النَّبِيِّ لَسْتُنَّ كَأَحَدٍ مِّنَ النِّسَاءِ ۚ إِنِ اتَّقَيْتُنَّ
فَلَا تَخْضَعْنَ بِالْقَوْلِ فَيَطْمَعَ الَّذِي فِي قَلْبِهِ
مَرَضٌ وَقُلْنَ قَوْلًا مَّعْرُوفًا ﴿٣٢﴾

33. Na kaeni majumbani mwenu, wala msionyeshe mapambo yenu kama walivyokuwa wakionyesha mapambo yao wanawake wa zama za Ujahili (Ujinga, ukafiri) na simamisheni Sala na toeni Zaka, na Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Mwenyezi Mungu Anataka kukuondoleeni uchafu, enyi watu wa nyumba (ya Mtume), na (anataka) kukutakaseni kabisa kabisa.

وَقَرْنَ فِي بُيُوتِكُنَّ وَلَا تَبَرَّجْنَ تَبَرُّجَ الْجَاهِلِيَّةِ
الْأُولَىٰ ۖ وَأَقِمْنَ الصَّلَاةَ وَآتِينَ الزَّكَاةَ وَأَطِعْنَ اللَّهَ
وَرَسُولَهُ ۚ إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيُذْهِبَ عَنكُمُ الرِّجْسَ
أَهْلَ الْبَيْتِ وَيُطَهِّرَكُمْ تَطْهِيرًا ﴿٣٣﴾

---

30. Mambo yanatengenea kwa wakubwa na yakaharibika kwa wakubwa. Wao ndio wanaofuatwa mwendo wao, ukiwa mwema au mbaya. Basi ndio wanaambiwa hapa wakeze Mtume — mabibi wa kuigwa — kuwa wakenda mwendo mbaya watalipwa kwa ukali zaidi kuliko wabaya wengine. Na wakenda mwendo mzuri watalipwa vizuri zaidi kuliko wema wengineo wote. Kila jambo linalipwa kwa kadiri ya athari yake.

31. Wakubwa kila siku ndio shabaha za wadogo katika kuwafuata. Wanalolifanya wakubwa ndilo linaloigwa; likiwa jema, likiwa baya, kwa kuwa watu wanaona kuwa hayo yanayofanywa na wakubwa ndio utamaduni, (ustarabu). Basi wanaiga; wajionyeshe kuwa na wao ni watamaduni waliotimu wasio na nukusani.

Ndio maana hao wakubwa wakajaziwa jaza kubwa kabisa za kheri wanapokwenda mwendo mzuri, kwani kwa njia hiyo wanaongoa chungu ya watu; na wakapewa ikabu kubwa zaidi wanapojipotoa kwani wengi wanawapotoa.

32. Ukubwa aliokupa Mwenyezi Mungu una zaka zake. Na moja katika zaka hizo ni kwenda mwendo mzuri, ikiwa si hivyo basi ikabu itakuwa kubwa. Na wanawake pambo lao kubwa kabisa ni kutua na kuchunga wao muruwa, wasiwe na chembe ya dowa wala towa. Na anayemuharibu mwanamke ni mwanamume. Shetani wa Binadamu ni Binadamu mwenziwe. Na mwanzo wa sababu ya kufanya maasi ya mwanamume na mwanamke ima kuonanana wakapendana au kusikia sauti wakaashikiana.

Ndio maana wanaambiwa wanawake hapa kuwa ikitokea dharura ya mwanamke kusemezana na mwanamume akaze sauti yake, asijesimeze kwa madaha; asije akavutika huyo mwenziwe kutaka kufanya mabaya naye. Na walivyoambiwa haya wakeze Mtume ndivyo wanaambiwa wanawake wengine wote.

33. Basi kama walivyokatazwa katika ile Aya ya pili kuzisikilizisha sauti zao ndivyo katika Aya hii wanavyokatazwa kuonyesha (a) Miili yao, (b) Mapambo yao.

Wanaambiwa wakae majumbani mwao, wasitoke ovyo ovyo. Watoke kwa dharura na haja tu. Ikiwa si hivyo basi wajikalie majumbani mwao wachunge muruwa wao.

34. Na watajieni (watu) yasomwayo majumbani mwenu katika Aya za Mwenyezi Mungu na (maneno ya) hikima (ya Mtume), kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa mambo ya siri na Mjuzi wa mambo ya dhahiri.

وَاذْكُرْنَ مَا يُتْلَىٰ فِي بُيُوتِكُنَّ مِنْ آيَاتِ اللَّهِ
وَالْحِكْمَةِ ۚ إِنَّ اللَّهَ كَانَ لَطِيفًا خَبِيرًا ﴿٣٤﴾

35. Bila shaka wanaume wenye kufuata vizuri nguzo za Uislamu, na wanawake wanaozifuata vizuri nguzo za Uislamu, na wanaume wanaoamini vizuri nguzo za Imani, na wanawake wanaoamini vizuri nguzo za Imani, na wanaume wanaotii, na wanawake wanaotii, na wanaume wasemao kweli, na wanawake wasemao kweli, na wanaume wanaosubiri, na wanawake wanaosubiri, na wanaume wanaonyenyekea na wanawake wanaonyenyekea, na wanaume wanaotoa (Zaka na) sadaka, na wanawake wanaotoa (Zaka na) sadaka, na wanaume wanaofunga, na wanawake wanaofunga, na wanaume wanaojihifadhi tupu zao, na wanawake wanaojihifadhi, na wanaume wanaomtaja Mungu kwa wingi, na wanawake wanaomtaja Mwenyezi Mungu (kwa wingi) Mwenyezi Mungu amewaandalia msamaha na ujira mkubwa.

إِنَّ الْمُسْلِمِينَ وَالْمُسْلِمَاتِ وَالْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ
وَالْقَانِتِينَ وَالْقَانِتَاتِ وَالصَّادِقِينَ وَالصَّادِقَاتِ وَ
الصَّابِرِينَ وَالصَّابِرَاتِ وَالْخَاشِعِينَ وَالْخَاشِعَاتِ وَ
الْمُتَصَدِّقِينَ وَالْمُتَصَدِّقَاتِ وَالصَّائِمِينَ وَالصَّائِمَاتِ وَ
الْحَافِظِينَ فُرُوجَهُمْ وَالْحَافِظَاتِ وَالذَّاكِرِينَ اللَّهَ كَثِيرًا
وَالذَّاكِرَاتِ أَعَدَّ اللَّهُ لَهُمْ مَغْفِرَةً وَأَجْرًا عَظِيمًا ﴿٣٥﴾

36. Haiwi kwa mwanamume aliyeamini wala kwa mwanamke aliyeamini, Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wanapokata shauri, wawe na hiari katika shauri lao. Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, hakika amepotea upotofu (upotevu) ulio wazi (kabisa).

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى اللَّهُ وَرَسُولُهُ
أَمْرًا أَنْ يَكُونَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ ۗ وَمَنْ يَعْصِ
اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالًا مُبِينًا ﴿٣٦﴾

---

Na ikitokea kutoka basi wasidhihirishe viwiliwili vyao wala vyombo vyao kama yalivyotajwa haya katika Aya hii na Aya ya 59 ya Sura hii na Aya ya 31 ya *Suratun Nur.*

Kila kiungo kilicho juu ya mwili wa mwanamke — na kila kilicho juu ya kiungo hicho, hata nywele — lazima kifinikwe kwa nguo, ila uso tu na vitanga (viganja) vya mikono. Na baadhi ya ulamaa wamesema "na nyayo." Na huo uso unaopewa ruhusa kuwa wazi, sharti usiwe umepambwa kwa kurembwa podari wala rangi za midomo wala za mashavu wala mapambo mengine na maremborembo mengine. Na hivyo vitanga vya mikono ndivyo vivyo hivyo.

Bali hata kusikilizana sauti ya vyombo alivyovaa isisikilizane, kama mabangili yake na mikufu yake na herini zake na mengineo yake; kama ilivyo katika Aya ya 31 ya *Suratun Nur.*

Basi seuze kusikilizana harufu ya manakato yake, licha kuonekana manukato hayo, kama wale wanaoonyesha mashada ya maasumini yao. Hao laana kubwa juu yao na juu ya waume zao na kamaa zao wengine wenye tasarufu juu yao.

Na anayejiwacha kubahashika atabahashiwa, asiwe na wa kumtetea wala kumlilia. Ugonjwa wa kujitakia hauambiwi pole.

Na kuambiwa wake zake Mtume ndio kuambiwa wanawake wote.

34. Na hapa wanahimizwa wanaojua wawafundishe wasiojua, wanaowajua na wasiowajua. Hakuna kazi bora zaidi kuliko kazi ya kuwafunza wasiojua na kuwazindua wasiotambua. Na hao wakeze Mtume wamezidiana daraja zao kwa wingi wa ile jitihadi ya kufundisha ilimu waliyoichukua. Mwenye daraja kubwa zaidi katika wake zake Mtume katika kazi ya kufundisha — isipokuwa Bibi Khadija na Bibi Zaynab bint Jahsh — ni Bibi Aysha, kisha Bibi Ummu Salama, khalafu Bibi Hafsa, tena Bibi Safiyya, na kama hivi.

Basi naajitahidi kila mmoja awe mfanye kheri na mfundishaji kheri.

36. Sababu ya kuteremka Aya hii ni kukataa Bibi Zaynab bint Jahsh kuolewa na Bwana Zaid bin Haritha. Huyu alikuwa huru wa Mtume, na Bibi Zaynab ni mtoto wa shangazi lake Mtume — Bibi Umayma. Basi yeye na

37 Na (Wakumbushe) ulipomwambia yule ambaye Mwenyezi Mungu amemneemesha (kwa kumuafikia Uislamu) na wewe ukamneemesha (kwa kumpa uungwana. Naye ni Bwana Zaid bin Haritha ulipomwambia): "Shikamana na mkeo na umche Mwenyezi Mungu (usimuache)" na ukaficha katika nafsi yako aliyotaka Mwenyezi Mungu kuyatoa (Nayo ni kuwa Mwenyezi Mungu amekuamrisha umuoe wewe huyo mkewe atakapomuacha ili iondoke ile itikadi iliyokuwa ikiitakidiwa ya kuwa mtoto wa kulea ni kama mtoto wa kumzaa), na ukawachelea watu, hali Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye haki zaidi ya kumchelea. Basi alipokwisha Zaidi haja yake na mwanamke huyo, Tulikuoza wewe ili isiwe taabu kwa Waislamu kuwaoa wale wa watoto wao wa kupanga wanapokuwa hawana haja nao. Na amri ya Mwenyezi Mungu ni yenye kutekelezwa.

وَإِذْ تَقُولُ لِلَّذِي أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِ وَأَنْعَمْتَ عَلَيْهِ
أَمْسِكْ عَلَيْكَ زَوْجَكَ وَاتَّقِ اللَّهَ وَتُخْفِي فِي نَفْسِكَ
مَا اللَّهُ مُبْدِيهِ وَتَخْشَى النَّاسَ وَاللَّهُ أَحَقُّ أَنْ
تَخْشَاهُ فَلَمَّا قَضَىٰ زَيْدٌ مِنْهَا وَطَرًا زَوَّجْنَاكَهَا لِكَيْ
لَا يَكُونَ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ حَرَجٌ فِي أَزْوَاجِ أَدْعِيَائِهِمْ
إِذَا قَضَوْا مِنْهُنَّ وَطَرًا وَكَانَ أَمْرُ اللَّهِ مَفْعُولًا ﴿٣٧﴾

38. Hapana lawama kwa Mtume katika (kufanya) yale ambayo Mwenyezi Mungu Amembainishia (hukumu yake): ndiyo kawaida ya Mwenyezi Mungu kwa wote waliopita zamani; na amri ya Mwenyezi Mungu ni mpango uliopangwa vizuri

مَا كَانَ عَلَى النَّبِيِّ مِنْ حَرَجٍ فِيمَا فَرَضَ اللَّهُ لَهُ
سُنَّةَ اللَّهِ فِي الَّذِينَ خَلَوْا مِنْ قَبْلُ وَكَانَ
أَمْرُ اللَّهِ قَدَرًا مَقْدُورًا ﴿٣٨﴾

39. Wale (Mitume waliopita kabla yako) waliokuwa wakifikisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu na kumuogopa wala hawamuogopi yo yote isipokuwa Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu ndiye Atoshaye kuhisabu.

الَّذِينَ يُبَلِّغُونَ رِسَالَاتِ اللَّهِ وَيَخْشَوْنَهُ وَلَا
يَخْشَوْنَ أَحَدًا إِلَّا اللَّهَ وَكَفَىٰ بِاللَّهِ حَسِيبًا ﴿٣٩﴾

40. Muhammad si baba wa yoyote katika wanaume wenu, bali yeye ni Mtume wa Mungu na Mwisho wa Mitume, Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.

مَا كَانَ مُحَمَّدٌ أَبَا أَحَدٍ مِنْ رِجَالِكُمْ وَلَٰكِنْ رَسُولَ اللَّهِ
وَخَاتَمَ النَّبِيِّينَ وَكَانَ اللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمًا ﴿٤٠﴾ ع

---

ndugu zake, wanaume na wanawake, walipinga jambo hili, wakaona ni kuvunjwa hishima yake kuolewa na huru wa ndugu yake. Lakini Uislamu hautazami mali wala nasabu, unamtazama yule mtu mwenyewe ulivyo mwendowake mwema na sifa zake nzuri na amali zake zenye nafuu. Hii ndio mizani. Basi Mtume alimpima mtumwa wake huyu na dada yake huyo; akawaona ni kufuu wa kuoana. Basi akasalimu amri akaolewa na huyo mtumwa; na hao ndugu zake wakasalimu amri wakatoa idhini. Basi huu ndio mwendo.

37. Katika kuamrisha jambo na kukataza intaka uwe wewe mwenyewe ndiye wa mbele kufuata; ikiwa si hivyo haitakuwa na nguvu amri hiyo wala katazo hilo. Na hapa ilikuwa kutolesha ruhusa kumuoa mwanamke aliyepata kuolewa na mtoto wa kulea. Na hapo zamani wakiona ni jambo la haramu kabisa, basi akaambiwa Mtume alifanye yeye mwenyewe kwanza.

39. Mwenyezi Mungu katuhimiza katika Qurani yote nzima kuwa tufuate mwendo wa watu wema. Na wa mbele ni Mitume. Basi mmoja katika mwendo wao hi huu wa Kutojali kubainisha haki, hata akikasirika nani na akavimbisha mashavu vipi.

40. *Khataman Nabiyyin* maana yake Mwisho wa Mitume, kinyume cha maneno ya uwongo ya Waahmadiyya, (Makadiani) waliojidai "Muhuri wa Manabii"! Na wakataja majina ya chungu ya wanavyuoni na vitabu vyao na KUSINGIZIA kuwa humo wamefasiri kama hivyo walivyofasiri wao. Si kweli. Ni KUDANGANYA tu huko. Hakuna tafsiri hiyo.

Tunasikitika na tunahuzunishwa na mwendo wanaokwenda wenye madhehebu ya Makadiyani. Wanajitahidi kuwatilisha watu shaka juu ya itikadi zao sahihi walizo nazo.

Wanajua na wana yakini kuwa Islamu wote wa kila madhehebu — tangu Uislamu ulipoanza mpaka leo — wanaitakidi na wanaandika katika kila kitabu kuwa Nabii Muhammad ndiye Mtume wa mwisho, hakuna atakayepewa Utume tena; kwani hivi ndivyo ilivyosema Qurani. Imesema *Khaatamana Nabiyyin* = Mwisho wa Mitume. Na ndivyo inavyosema pia *Minqablika* = Waliopewa Utume kabla yako. Hakuna katika Qurani *Minbaadika* = Watakaopewa Utume baada yako. Na ndivyo zilivyosema dhahiri shahiri Hadithi za Mtume sahihi zilizomo katika vitabu vyote vya Hadithi kuwa *Laa Nabiyya Baady* = Hapana atakayepewa Utume baada yangu. Hapana kimoja kilichokhalifu haya, kikasema kwamba Uislamu unakubalisha kuwa atapata Utume mtu mwengine baada ya Nabii Muhammad. Wanajua wakubwa wao kwa yakini kuwa hapana kitabu cha Uislamu kinachosema hivyo, kabla ya kusema wao haya. Yakini wanayo kuwa hapana kitabu cha Uislamu kinachotegemewa kinachosema hivyo. Lakini wanataka kuwatia shaka tu watu na wasiwasi katika itikadi zao zilizo sahihi, wawatoe katika Uislamu.

Kwa hivyo wameandika katika paragraph ya 6 sahifa 737 ya tafsiri yao kuwa imeandikwa katika Addurrul Manthuur kuwa Bibi Aysha amesema: "Semeni yeye ni *Khaataman Nabiyyin* lakini msiseme kuwa hakuna Nabii baada yake." Wameandika hivi ili kuonyesha kuwa Bibi Aysha anasema, kama wanavyosema wao, "kuwa Nabii Muhammad si Mtume wa mwisho, watapata Utume watu wengine pia." Nayo sivyo kabisa. Hakusema hivyo Bibi Aysha; wala Islamu yoyote mwengine. Muradi wa Bibi Aysha kwa maneno hayo umebainishwa papo hapo katika Addurrul Manthuur baada ya mstari mmoja tu, katika Hadithi ya Sahaba Mughyra bin Shuuba kuwa "Semeni yeye *Khaataman Nabiyyin* = Mtume wa mwisho. Lakini msisema *Laa Nabiyya baadahuu* = Hapana Mtume baada yake, kwani Sisi tukisimliwa (na Mtume) kuwa Nabii Isa atarejea. Basi yuko Mtume atakuja hapa ulimwenguni baada yake, lakini alipewa Utume kabla yake, naye ni Nabii Isa.

Basi hii ndiyo sababu ya kukataza Bibi Aysha kusema *Laa Nabiyya baadahuu* na kukataza Bwana Mughyra bin Shuuba, si hivyo walivyodhanisha wao kuwa huyu Bibi Aysha anaitakidi kuwa atapata mtu mwingine Utume baada ya Nabii Muhammad. Haitakidi Bibi Aysha hivyo, kama yalivyobainishwa haya papo hapo katika sahifa hiyo ya 204 ya hiyo tafsiri ya Al Imam As Suyuty inayoitwa Ad Durrul Manthuur, ambayo wao wamechukuwa huo mstari wa kati, wakautupa mstari ulioko chini yake; na wakaitupa vile vile mistari yote iliyo juu yake katika sahifa hiyo ya 204 ya Ad Durrul Manthuur. Mistari ya juu yake yote ya sahifa hiyo imethubutisha Hadithi sahihi zilizopokewa na Imam Ahmad, Imam Al Bukhary, Imam Muslim, Imam Abu Daud, Imam Attirmidhy, Imam An Nasai, Imam Ibn Majah na wengineo kuwa Mtume ni *La Nabiyya Baadahuu* = Hapana atakayepata Utume baada yake; na *Aakhiru Nabiyy* = Mtume wa mwisho kupata Utume; na *Aakhiru Man Buitha* = Wa mwisho kupewa Utume.

Basi katika tafsiri yao si wanafanya maksudi kuwashawishi watu katika itikadi zao, ili wafuate hivyo wanavyoitakidi wao? Na hali ya kuwa hivyo sivyo, kama ilivyobainishwa humo katika sahifa 204 ya juzuu 5 ya Ad Durrul Manthuur.

Na vile vile wamesema katika paragraph ya 2 ya sahifa 738 ya hiyo tafsiri yao kuwa imo katika kitabu cha Imam Ibn Majah kuwa Mtume amesema "Angeishi Ibrahimu angekuwa Nabii mkweli." Wameandika haya ili kuonyesha kuwa Mtume amejawizisha kuwa watapata Utume watu wengine baada yake. Na hali ya kuwa Mtume hakukubalisha kabisa jambo hili wala Mwenyezi Mungu. Bali Mwenyezi Mungu amekataa kabisa haya kwa kusema (a) *Minqablika* = Waliopewa Utume kabla yako, na kusema (b) *Wakhaataman Nabiyyina* = Yeye (Nabii Muhammad) ndiye mwisho wa Mitume. Na akakataa mwenyewe Mtume kwa kusema *Laa Nabiyya baady* = Hatapata Utume mtu baada yangu. Na hiyo Hadithi ya Imam Ibni Majah waliyoitaja imebainishwa humo humo katika hicho hicho kitabu cha Ibni Majah katika sahifa hiyo hiyo ya 237 ya juzuu ya kwanza kuwa hiyo si Hadithi barabara, bali: *Dhaif* = Haina nguvu. Wameona imeandikwa hivyo humo. Na wameona katika kitabu cha *Asnal Matalib Fy Ahaadyth Mukhtalifatil Maraatib* katika sahifa 176 kuwa hiyo ni *Hadythun Baatil* = Hadithi ya uwongo. Na wameona katika kitabu cha Imam An Nawawy katika sahifa 193 ya juzuu ya awali kinachoitwa *Tahdhybul Asmaa*, vile vile, kuwa Hadithi hiyo ni ya uwongo = *Hadythun Baatil.*

Basi Hadithi batili ndiyo ya kutolea stishhadi? Na hali ya kuwa papo hapo katika hiyo sahifa 237 ya juzuu hiyo ya kwanza ya kitabu hicho cha Ibni Majah imetajwa Hadithi sahihi ambayo hata Imam Al Bukhary na wengine wameitaja. Nayo *Laa Nabiyya baadahuu* = Hapana atakayepata Utume baada yake (Nabii Muhammad). Katika mstari wa mwanzo wa sahifa hii 237 ya kitabu cha Ibni Majah, imetajwa Hadithi hii sahihi. Wao wameiruka, wameiendea Hadithi batili iliyomo katika mstari wa 4!

Basi ndiyo haki hii wenye dini hiyo kutaka kuwashawishi watu makusudi na kuwapoteza? Bali katika sahifa hiyo hiyo ya 237 ya hicho kitabu cha Ibni Majah imeandikwa kwa urefu wake hiyo Hadithi waliyotaja wao kwa ufupi wake tu, ili wawadhanishe watu kuwa Mtume na ulamaa wa Kiislamu wanakubalisha kuwa watapata Utume watu wengine baada ya Nabii Muhammad. Nao sivyo kabisa. Hakuna waliosema hayo. Basi urefu wa ile Hadithi ya Ibni Majah waliyoitaja wao ambayo iko katika sahifa 237 ya hicho kitabu cha Ibni Majah; urefu wake ni huu alioutaja Imam Ibni Man-dah ulioko katika sahifa hiyo hiyo ya 237 ya kitabu hicho cha Ibni Majah ambao ni: "Lau angesalia Ibrahimu nyuma ya Mtume angekuwa Mtume, lakini muhali kusalia hai baada ya Mtume kwani

Mtume wenu huyu (Nabii Muhammad) ndiye Mtume wa mwisho." Basi mbona wamekiruka kipande hiki cha kuonyesha kuwa muhali kuja Mtume baada ya Nabii Muhammad? Si insafu wanavyofanya: wanamegua huku wakimegua huku, ili waigeuze sura ya kitu kiwe chengine! Lakini *Alhamdu Lillah;* tumeiona mimeguo yote hiyo, tukairejesha mahala pake, yakarejea hayo maneno katika sura yake. Na kama wanvyomeguamegua wakatafuniatafunia wakati mwengine, ndivyo wanavyopachikiapachikia visivyokuwapo wakati mwengine. Na yote haya ili kuwababaisha watu na kutaka kuwatoa katika Uislamu wao.

Basi haifai kabisa kuamini nakla (quotations) wanazozitaja. Hawaziandiki kwa uaminifu hata kidogo — wanamegua, wakayatoa yaliyoko, wakabandikia wakatia yasiyokuwapo; kisha wakasingizia kuwa amesema Fulani. Khatari kubwa! Tusiwaamini mpaka tuone kwa macho yetu. Wala hatutaona hata siku moja kitabu cha Muislamu anayekubalisha kuwa atapata Utume mtu mwingine, baada ya Nabii Muhammad. Na tunawahadharisha na adhabu kubwa kabisa ya Mwenyezi Mungu inayowangoja wanaopoteza watu makusudi.

Na katika matamko waliyoyakoroga ni tamko la *Khaataman Nabiyyina* katika mstari wa 18 na wa 47 wa sahifa 735. Walisema *Khaataman Nabiyyina* (Muhuri wa Manabii). Tunasema sisi kwamba hakuna mfasiri yoyote tangu Qurani ilipoanza kufasiriwa hizo zama za Mtume na Masahaba mpaka hivi sasa (ila wao) aliyefasiri *Khaataman Nabiyyina* kwa kuwa "Muhuri wa Manabii," si Mtume wa mwisho. Na watuonyeshe kitabu hicho kabla ya hivi vitabu vyao walivyovitunga wao wakapachikiza itikadi yao hiyo ya wao peke yao, wasiokuwa na wenziwao. Itikadi ya ukafiri. Wallahi hawakipati. Wanawavunganyiza tu watu kwa hayo wayasemayo na wayaandikayo.

Tena wakasema kwenye huo mstari wa 47 wa sahifa 735: "Neno Khatam katika lugha ya Kiarabu lina maana ya muhuri." Wameandika hivi ili kudhanisha watu kwamba maana ya Khatam katika Kiarabu ni hiyo tu ya muhuri, na hali ya kuwa tamko la Khatam lina maana: (1) Muhuri, (2) Pete, (3) Kizibo, (4) Wa mwisho, (5) Kidimbwi kilioko nyuma ya shingo na, (6) Weupe wa miguu ya farasi. Tafsiri hizi hata mwenye kamusi, (dictionary) linaloitwa Al Munjid amezitaja, ambaye yeye hata si Islamu. Nawatazame tamko la Khaatam katika hiyo Al Munjid wataona tafsiri hizo zote. Na hilo tamko la Khaatam lina tafsiri nyingine pia zisizokuwa hizi. Lakini hawataona katika kamusi lolote la lugha ya Kiarabu lililofasiri tamko la *Khaataman Nabiyyin* kuwa "Muhuri wa Manabii tu, si Mtume wa mwisho." Katu hawataiona tafsiri hii. Wote watawaona wamelifasiri mara moja kwa maana ya "Mtume wa mwisho" au wamelifasiri kwa kuwa "yeye ndiye aliyewapamba Mitume kwa utukufu wake na kwa kuwa yeye Mtume wa mwisho" au kuwa "yeye ndio muhuri aliofungia Mwenyezi Mungu Utume kuwa hapana tena." Lakini kuwa maana yake ni "Muhuri wa Mitume tu, si wa mwisho wao" — hawataona kabisa.

A. Tukichukuwa makamusi mashuhuri ya kufasiri lugha ya Kiarabu tutamuona:

(1) Mwenye Al Mukhtar amesema katika sahifa 169: "*Khatima* ya kitu ni mwisho wake; na Nabii Muhammad ni mwisho wa Mitume."

(2) Mwenye As Sahaah amesema katika sahifa 28 ya juzuu ya pili vivi hivi neno kwa neno.

(3) Mwenye Tajul Aruus katika sahifa 267 ya juzuu ya 8 amesema: "*Khaataman Nabiyyin* maana yake wa mwisho wao."

(4) Mwenye Lisaanul Arab katika sahifa 55 ya juzuu ya 15 amesema: "*Khaataman Nabiyyin* maana yake wa mwisho wao."

Basi wanavyuoni wote hawa wa lugha ya Kiarabu hawajui maana ya *Khaataman Nabiyyina* ila wao?

B. Tukichukuwa makamusi yanayofasiri lugha iliyomo katika Hadithi za Mtume tutamuona:

(1) Mwenye Majmai Bihaaril Anwar katika sahifa 330 ya juzuu ya kwanza amesema "*Khaatam* na *Khaatim* ni katika majina ya Mtume . . . maana yake wa mwisho wao (Mitume)."

(2) Mwenye Hadyus Saary katika sahifa 108 amesema: "*Khaataman Nabiyyin* maana yake wa mwisho wao (Mitume)."

Basi wanavyuoni hawa waliokubaliwa na watu wote kuwa ni wajuzi wa lugha aliyoitumia Mtume katika Hadithi zake, hawakuijua maana ya kweli kweli ya *Khaataman Nabiyyina*, mpaka waijue sasa watu wa kijiji kidogo cha Bara Hindi?

C. Tukichukuwa makamusi yanayofasiri lugha iliyomo katika Qurani tutamuona:

(1) Mwenye Al Mufradaat katika sahifa 142 anasema: "*Khaataman Nabiyyina* kwa sababu yeye ameumaliza Utume yaani ameutimiza kwa kuja kwake; hatakuja mwingine."

(2) Mwenye Gharybul Qurani katika sahifa 100 anasema: "*Khaataman Nabiyyina* ni mwisho wa Manabii " Basi wanavyuoni hawa waliokubaliwa na Waislamu wote kuwa ni wajuzi wa Kiarabu alichokitumia Mwenyezi Mungu katika Qurani, hawakuweza kujua maana ya *Khaataman Nabiyyina* ila imejulikana sasa na watu wa kijiji cha Bara Hindi?

D. Tukichukua tafsiri za Qurani tutaona:

(1) Tafsiri ya Sahaba Ibnu Abbas katika sahifa 262 inasema: "*Khaataman Nabiyyina* ni kuwa Mwenyezi

Mungu amewamaliza kwake Mitume waliokuja kabla yake, basi hatakuwa mtu mwingine atakayepata Utume baada yake."

(2) Tafsiri ya Imam Ibni Jarir katika sahifa 11 ya juzuu ya 21 inasema: "*Khaataman Nabiyyina* kwa kuwa amemaliza Utume, akaupiga muhuri, basi hautafunguliwa kupewa yoyote mpaka siku ya Kiama."

(3) Tafsiri ya Imam Annaysabury katika sahifa 15 ya juzuu ya 21 inasema: "*Khaataman Nabiyyina* kwa kuwa hapana atakayepata Utume baada ya Nabii Muhammad."

(4) Tafsiri ya Imam Ibni Kathir katika sahifa 492 ya juzuu ya 3 inasema: "Aya hii (yenye *Wakhaataman Nabiyyina)* inaonyesha wazi wazi kuwa hapana atakayepata Utume baada yake . . . Na Hadithi nyingi kabisa zilizopindukia hadi zimepokewa kwa Mtume juu ya habari hii (kuwa yeye ni Mtume wa mwisho)."

(5) Tafsiri ya Imam Ashshawkaany katika sahifa 276 ya juzuu ya 4 inasema: "*Khaataman Nabiyyina* kuwa amekuja mwisho wao wote."

(6) Tafsiri ya Al Kashshaf ya Imam Azzamakhshary katika sahifa 215 ya juzuu ya pili inasema: "*Khaataman Nabiyyina* maana yake mwisho wa Manabii."

(7) Tafsiri ya Imam Al Baydhawy katika sahifa 559 inasema: "*Khaataman Nabiyyina* ni wa mwisho wao aliyemaliza au waliyomalizwa kwake yeye . . . wa mwisho kupewa Utume."

(8) Tafsiri ya Imam Al Khazin kwenye sahifa 18 ya juzuu ya tatu imeandika: "*Khaataman Nabiyyina* maana yake ameukhatimisha Mwenyezi Mungu Utume kwake yeye (Nabii Muhammad). Hapana tena kupewa mtu Utume baada yake."

(9) Tafsiri ya Imam Anaasafy katika sahifa 473 ya juzuu ya pili imeandika: "*Khaataman Nabiyyina* maana yake wa mwisho wao. Hatapewa Utume mtu mwingine baada yake."

(10) Tafsiri ya Imam Al Baghawy katika sahifa 718 ya juzuu ya pili imesema: "*Khaataman Nabiyyina* ni wa mwisho wao."

(11) Tafsiri ya Ruuhul Bayan ya Imam Ismail katika sahifa 122 ya juzuu ya tatu imesema: "*Khaataman Nabiyyina* kwa kuwa wa mwisho wao (Mitume); waliomalizika kwa kuja yeye."

(12) Tafsiri ya Ruuhul Maany ya Imam Al Alusy katika sahifa 32 ya juzuu ya 22 inasema: "*Khaataman Nabiyyina . . . Aakhirun Nabiyyin* = Mwisho wa Mitume."

(13) Tafsiri ya Jalaleyn ya Imam Al Mahally katika sahifa 234 ya juzuu ya 3 ya Hashiya ya Imam Assawy imeandika: "*Khaataman Nabiyyina* kwa kuwa hapana atakayepewa Utume baada yake."

(14) Tafsiri ya Jalaleyn katika sahifa 442 ya juzuu ya 3 ya Hashiya ya Imam Al Jamal imesema: "*Khaataman Nabiyyina* kwa kuwa hatapewa Utume mtu mwingine baada yake." Na wafasiri wengine wote wa Kiislamu wamesema hivi.

Wakaendelea kuikoroga tafsiri ya *Khaataman Nabiyyina* katika mstari wa 48 wa hiyo sahifa 735 ya tafsiri yao. Wakasema "Inasimuliwa ya kuwa siku moja Mtume s.a.w. alinuia kuandika barua za kuwabashiri Wafalme, na Masahaba wakasema ya kwamba Wafalme wa Kiajemi hawapokei barua mpaka iwe na muhuri wa muandikaji. Mtume s.a.w. alitengenezesha Khaatam, na juu yake yakaandikwa maneno: Muhammad Mtume wa Mungu (Bukhari na Muslim)."

Tunasema sisi kwamba hapana mtu anayekataa akasema kuwa Mtume hakufanya muhuri alipoambiwa kwamba barua zake atakazowapelekea Wafalme hazitakubaliwa mpaka azitie muhuri, kama tunavyoona sisi hapa na kila mahali, mikataba na barua muhimu na maandishi muhimu yanatiwa muhuri ili kuonyesha kuwa hayo ni thabiti, yametokana nao. Basi Mtume alipotengeneza muhuri wa kutia katika barua zake na mikataba yake, ndiyo amekuwa *Khaataman Nabiyyina*, "Muhuri wa Manabii." Hawawachi kujidanganya na kutaka kudanganya watu! Basi mtu akifanya muhuri ndio atakuwa na mwenyewe muhuri? Akiwa Mtume awe muhuri wa Mitume! Akiwa Mfalme awe muhuri wa Wafalme! Akiwa Shekhe awe muhuri wa mashekhe! Maneno gani jama haya?

Na huko kuandika kwao: (Bukhari Jalda I: Muslim Kitaabul Libaas) ili kuonyesha kuwa stish-hadi hii ya kuwa Mtume kaitwa *Khaataman Nabiyyina* kwa kuwa maana yake Muhuri wa Manabii imo katika kitabu cha Imam Al Bukhary na Imam Muslim. Nao ni uwongo kabisa. Hawakusema itikadi hii, la Bukhary wala Muslim wala mwinginewe yoyote aliye Mwislamu.

Wenyewe wamejipalia makaa hapa. Wamesema (Muslim, Kitaabul Libaas). Yaani Muslim ameitaja habari hii katika kitabu chake katika mlango wa Kitabullibasi. Maana yake kama kila mtu anavyojua ni kuwa mlango huo unataja mavazi aliyokuwa akivaa Mtume, na moja katika mavazi hayo ni pete yenye muhuri wake. Basi mlango huo, kama wanavyoona, ameuweka Imam Muslim kwa kuonyesha kuwa Mtume akivaa mavazi namna fulani, na moja katika mavazi hayo ni pete. Hakuuweka mlango huo kwa kuonyesha kuwa ameitwa *Khaataman Nabiyyina* kwa ajili ya hiyo pete ya muhuri wake anayoivaa. Uko wapi mlango namna huo katika Sahihi Muslim au kwengineko? Basi si kumsingizia uwongo tu hivyo Imam Muslim na kumsambikiza kusema kitu asichokisema? Nawautazame mlango huu katika sahifa 324 ya juzuu ya 3 ya hiyo Sahihi Muslim, wataona hivi tulivyosema sisi kuwa ameutaja mlango huu kwa ajili ya kuonyesha namna Mtume alivyokuwa akivaa.

Na alipotaka Imam Muslim kulifasiri tamko la *Khaataman Nabiyyina* aliliwekea mlango wake katika mstari wa

16 katika sahifa 59 ya juzuu ya 4 ya kitabu chake hiki kinachojulikana kwa jina la Sahihi Muslim, akalifasiri *Khaataman Nabiyyina* kama walivyolifasiri Waislamu wote — kuwa maana yake ni Mtume wa mwisho, aliyekuja mwisho wa Mitume yote. Na wao wameona humo; lakini basi tu wanajitia pambani. Na wameona pia katika hiyo juzuu ya 4 katika sahifa 82 Hadithi ya Mtume iliyosema: "Baada yake hatapata mtu mwingine Utume."

Na katika hiyo Jalada 1 ya kitabu cha Imam Al Bukhary, wanaona ile Hadithi ya kuwa Mtume amefanya muhuri tu, lakini hawakuona tafsiri ya *Khaataman Nabiyyina* iliyomo humo katika faslu ya "Mlango wa kubainisha nini maana ya *Khaataman Nabiyyina?*" Hawakuuona mlango huu? Wala namna alivyofasiri Al Bukhary — kama Waislamu wenziwe — kuwa muradi wa *Khaataman Nabiyyina* kuwa Mtume Muhammad ndiye Mtume wa mwisho? Hawakuona mlango huu katika hiyo Jalada 1 ya Sahihi Bukhary? Au wanajitia pambani zao tu ili wawakufurishe Waislamu? Au hawakuona katika hiyo hiyo jalada ya awali ya Sahihi Bukhari katika mstari wa 37 wa sahifa 173 Hadithi aliyoitaja huyu Imam Al Bukhary kwamba Mtume amesema maneno haya: "Hakitafika Kiama kabla ya kuja wazushi waongo kiasi ya 30 hivi: kila mmoja anajidai kuwa yeye ni Mtume wa Mwenyezi Mungu?" Hawajaona Hadithi hii humo katika Al Bukhari na mwingineko? Mbona wanasema kuwa huyo mtu wao ni Mtume? Na Mtume amesema atakayejidaia Utume baada yake ni muongo mzandiki! Basi wao katika vitabu hawaoni yale ya haki wasioitaka, ila huona yake maneno ambayo wakitaka kuyasopotoa husopotoka! Na Mwenyezi Mungu amekataza sana mtindo huu wa kusopotoa maneno, akasema katika Aya ya 78 ya *Aali Imran:* "Wanazisopotoa ndimi zao katika kufasiri maneno ya vitabu vya Mwenyezi Mungu ili muyadhani (hayo wanayoyasema wao) kuwa yamo ndani ya vitabu hivyo, wala hayamo katika vitabu hivyo. Na wanasema kuwa hayo yanatokana na Mwenyezi Mungu, wala hayatokani na Mwenyezi Mungu. Wanamsingizia uwongo tu Mwenyezi Mungu, na wao wanajua kuwa wanamsingizia uwongo."

Kila aliyesoma tafsiri ya Qurani anajua kwamba Aya hii: *Wakhaataman Nabiyyin* imeteremka wakati Mtume alipomuoa Bibi Zainab bint Jahsh. Na kila mwenye kusoma tarekhi ya Mtume anajua kwamba Mtume alimuoa Bibi Zainab katika mwaka wa tano wa Al Hijra au kabla ya hapo. Na kila mwenye kusoma tarekhi ya Mtume anajua vile vile kwamba Mtume alianza kuwapelekea barua hao wafalme mwisho wa mwaka wa sita na mwanzo wa mwaka wa saba.

Basi mbona alitajwa kwa sifa ya *Khaataman Nabiyyin* katika Aya ya 40 ya *Suratil Ahzab*, nayo ilikuja kabla ya kufua kwake Mtume huo muhuri? Si moja hii katika alama za uwongo wa tafsiri yao hiyo kuwa ameitwa *Khaataman Nabiyyin* kwa ajili ya muhuri aliofua zama za kuwapelekea barua wafalme! Na muhuri huo umefuliwa baada ya kupita myaka miwili tangu kuteremka Aya hii.

Na hilo porojo lao walilolianza tangu katika mstari wa 20 sahifa 736 ya tafsiri yao juu ya kutaja kuwa Mtume amekataza kuvaa pete ya dhahabu na . . . halikhusiani kitu na haya tuliyo nayo. Hiyo ni farumu ya bure tu wanayoitia. Nani asiyekubali kuwa Mtume amewakataza wanaume kutumia mapambo ya dhahabu na mavazi ya hariri?

Na chuku (uwongo) nyingine waliyoipiga katika kusingizia kuwa *Khaataman Nabiyyina* maana yake pambo la Mitume, ni kusema kwao katika mstari wa 34 wa sahifa 736 kuwa: "Amefanywa pambo kwa ajili ya Manabii. Kama Mtume Muhammad s.a.w. asingefika duniani Manabii wasingepata kupambwa, kwa kuwa wamepewa sifa mbaya katika vitabu vya Mayahudi na Wakristo . . ." Hawawachi! Mitume wote wamepewa sifa mbaya katika vitabu vya Mayahudi na Wakristo? Wanajua kuwa haya ni uwongo, lakini basi tu wanatia ngwenjera ili wawakufurishe Waislamu.

Na huku kutia kwao katika mstari wa 57 wa sahifa 736 matamko ya *Mudhaf na Mudhafilahyi*, ni vunganyizo tu hizo za kuyafanya maneno hayo yawe yana kima, (maana); kumbe hayana kima hata cha pesa mbili — kama kelele za goma bovu. Na goma bovu ndilo lenye kelele mbovu.

Na katika maneno yao ya uwongo kabisa na haya yaliyoko katika mstari wa 40 wa sahifa 738 kuwa "Watu wasio na maarifa wanafahamu kuwa Mtume s.a.w. ni *Khaatam* kwa maana ya kuwa amekuja mwisho wa Manabii . . ." Hawawachi! Wasiokuwa na fahamu ndio wanaosema hivi! Na hali ya kuwa wanavyuoni wote wamesema hivyo. Wanavyuoni wa lugha ya Kiarabu ya dasturi, na wa lugha ya Kiarabu ya Qurani na wa lugha ya Hadithi za Mtume, na wanavyuoni wa kufasiri Qurani! Unatosha uwongo wao hapa. Uwongo wao Umetia Maji Maziwani.

Na makala zao hizo walizowatajia Maimamu hawa: Assuyuuty, Ashshaarany, Arrazy na kadhalika ni uzushi mtupu na usingizio tu, kama walivyofanya katika mara za kwanza, na ndivyo watavyokuwa wanafanya maisha, kwani hawana pa kukamatia. Na itakuwa kazi kubwa na kujaza makaratasi bure tukitaka kuirejesha kila misingizio hii ya sasa pia mahala pake.

Sisi tuko tayari saa watakayo wakutane na sisi mbele ya khalaiki ya watu, watuonyeshe nafsi za ibara za Maimamu hawa zinazosema kuwa: *Nabii Muhammad si Mtume wa mwisho. Walipata—au watapata—Utume baada yake wengine au mwingine mmoja tu.* Tuko tayari saa watakayo wakutane na sisi mbele ya khalaiki ya watu watuonyeshe.

Na maadamu tumekwishadhihirisha tafsiri za kweli na tumefedhehesha zile singizio zao zilizopita, tunaona kuwa inatosha. Tupumzishe kalamu zetu kidogo, tuburudishe bongo vile vile kwa mengine. Kitu hicho kwa hicho

41. Enyi mlioamini! Mkumbukeni Mwenyezi Mungu kwa wingi

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ ٱذْكُرُوا۟ ٱللَّهَ ذِكْرًا كَثِيرًا ﴿٤١﴾

42. Na Mtukuzeni asubuhi na jioni.

وَسَبِّحُوهُ بُكْرَةً وَأَصِيلًا ﴿٤٢﴾

43. Yeye ndiye Anayekurehemuni; na Malaika Wake (wanakuombeeni dua); ili kukutoeni katika giza (kwa kukupelekeni) katika nuru, naye ni Mwenye kuwarehemu sana Waislamu.

هُوَ ٱلَّذِى يُصَلِّى عَلَيْكُمْ وَمَلَٰٓئِكَتُهُۥ لِيُخْرِجَكُم مِّنَ
ٱلظُّلُمَٰتِ إِلَى ٱلنُّورِ ۚ وَكَانَ بِٱلْمُؤْمِنِينَ رَحِيمًا ﴿٤٣﴾

44. Maamkiano yao siku ya kukutana naye yatakuwa (ya salama na) Amani, na Amewaandalia malipo matukufu.

تَحِيَّتُهُمْ يَوْمَ يَلْقَوْنَهُۥ سَلَٰمٌ ۚ وَأَعَدَّ لَهُمْ أَجْرًا
كَرِيمًا ﴿٤٤﴾

45. Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Kwa yakini Sisi Tumekutuma, (tumekuleta uwe) shahidi na Mtoaji wa habari nzuri, na Muonyaji

يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّبِىُّ إِنَّآ أَرْسَلْنَٰكَ شَٰهِدًا وَمُبَشِّرًا وَ
نَذِيرًا ﴿٤٥﴾

46. Na uwe muitaji (wa watu) kwa Mwenyezi Mungu, kwa idhini Yake, na (uwe) taa itoayo nuru.

وَدَاعِيًا إِلَى ٱللَّهِ بِإِذْنِهِۦ وَسِرَاجًا مُّنِيرًا ﴿٤٦﴾

47. Na wape habari njema Waislamu ya kwamba wana fadhila kubwa itokayo kwa Mwenyezi Mungu.

وَبَشِّرِ ٱلْمُؤْمِنِينَ بِأَنَّ لَهُم مِّنَ ٱللَّهِ فَضْلًا
كَبِيرًا ﴿٤٧﴾

48. Na usiwatii makafiri na wanafiki, wala usijali udhia wao; na mtegemee Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa Mlinzi.

وَلَا تُطِعِ ٱلْكَٰفِرِينَ وَٱلْمُنَٰفِقِينَ وَدَعْ أَذَىٰهُمْ وَتَوَكَّلْ
عَلَى ٱللَّهِ ۚ وَكَفَىٰ بِٱللَّهِ وَكِيلًا ﴿٤٨﴾

---

huchosha. Na sisi hatutaki kuwachosha tunaotaka kuwanabihisha. Na tanbihi ndogo tu humtosha mwenye akili.

Hapa ndio mwisho wa hiki kipande kidogo cha kuwabainishia Waislamu ubaya uliyomo katika tafsiri ya *Khaataman Nabiyyina* waliyoifasiri. Lazima wahadharishwe Waislamu ubaya wa tafsiri hiyo au itawatoa Uislamuni — wawe Murtadi — wakiamini baadhi ya yaliyomo katika maelezo ya tafsiri ya *Khaataman Nabiyyina.*

Sisi sana tumewabana katika ule uwongo wao wa kumdaia kwao Utume huyo mtu wao; na tukawabana sana vile vile katika kupindua kwao tafsiri ya hiyo *Khaataman Nabiyyina,* na tukawabana sana kadhalika katika kuwasingizia wanavyuoni maneno wasiyoyasema ili wazidi kuwapoteza watu; kwani watu wakiona kuwa "Shekhe Fulani amesema hivi" wanasadiki, na hali ya kuwa ni uwongo kabisa huo, hawakusema mashekhe hao haya kabisa; huo ni uzushi wao tu wanaowazushia mashekhe hao na vitabu hivyo na kumzulia Mwenyewe Mwenyezi Mungu na Mtumwwe. Na huo ni upotofu mkubwa na upotezaji usiokuwa na mfano.

Mwenyezi Mungu amewakanushia Uislamu watu wanaomsingizia Mungu na kusingizia watu mambo wasiyoyafanya wala wasiyoyasema. Akasema Mwenyezi Mungu katika Aya ya 105 ya *Suratin Nahl:* "Wanaozua uwongo ni wale wasioziamini Aya za Mwenyezi Mungu, na hao ndio waongo." Basi hao watakuwa na adhabu ya kuhiziwa na kuhizika hapa duniani, na Akhera watiwe Motoni, kama anavyosema Mwenyezi Mungu katika Aya ya 152 ya *Suratul Aaraf* kuwa: "Zitawafikia ghadhabu zinazotoka kwa Mola wao na fedheha kubwa katika maisha yao haya ya dunia; na hivi ndivyo tunavyowalipa wazushi." Kamba ya mwongo fupi, maisha haimfungii uzuri mirundi ya uwongo wake. Mwenyezi Mungu anasema katika Aya ya 61 ya *Surat Taha:* "Na hatengenekewi anayezua uwongo."

49. Enyi mlioamini! Mtakapowaoa wanawake; wenye kuamini kisha mkawapa talaka kabla ya kuwagusa, basi hamna eda juu yao mtakayoihisabu. Na wapeni cha kuliwaza na muwawache muachano mzuri.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِذَا نَكَحْتُمُ الْمُؤْمِنَاتِ ثُمَّ
طَلَّقْتُمُوهُنَّ مِنْ قَبْلِ أَنْ تَمَسُّوهُنَّ فَمَا لَكُمْ
عَلَيْهِنَّ مِنْ عِدَّةٍ تَعْتَدُّونَهَا ۖ فَمَتِّعُوهُنَّ
وَسَرِّحُوهُنَّ سَرَاحًا جَمِيلًا ﴿٤٩﴾

50. Ewe Nabii! Tumekuhalalishia wake zako uliowapa mahari yao, na (wanawake) uliowatamalaki kwa mkono wako wa kulia katika wale Aliokupa Mwenyezi Mungu, na (tumekuhalalishia) mabinti wa ami zako na mabinti wa mashangazi yako, na mabinti wa wajomba zako na mabinti wa dada za mama zako, waliohama pamoja nawe; na (tumekuhalalishia kila) mwanamke Mwislamu akijitoa mwenyewe bure kwa Mtume, kama mwenyewe Mtume akitaka kumuoa. Ni halali kwako tu (kumuoa mwanamke bure bila ya mahari) si kwa Waislamu wengine. Bila shaka Tumekwishabainisha Tuliyowafaridhia wao katika wake zao na wanawake iliyowatamalaki mikono yao ya kulia. (Tumekufanyizia hivi peke yako wewe Mtume tu) ili isiwe dhiki kwako (ukitaka kumuoa mwanamke mwengine kwa ajili ya kutangaza dini). Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ إِنَّا أَحْلَلْنَا لَكَ أَزْوَاجَكَ اللَّاتِي آتَيْتَ
أُجُورَهُنَّ وَمَا مَلَكَتْ يَمِينُكَ مِمَّا أَفَاءَ اللَّهُ عَلَيْكَ
وَبَنَاتِ عَمِّكَ وَبَنَاتِ عَمَّاتِكَ وَبَنَاتِ خَالِكَ وَبَنَاتِ خَالَاتِكَ
اللَّاتِي هَاجَرْنَ مَعَكَ وَامْرَأَةً مُؤْمِنَةً إِنْ وَهَبَتْ
نَفْسَهَا لِلنَّبِيِّ إِنْ أَرَادَ النَّبِيُّ أَنْ يَسْتَنْكِحَهَا خَالِصَةً
لَكَ مِنْ دُونِ الْمُؤْمِنِينَ ۗ قَدْ عَلِمْنَا مَا فَرَضْنَا
عَلَيْهِمْ فِي أَزْوَاجِهِمْ وَمَا مَلَكَتْ أَيْمَانُهُمْ لِكَيْلَا يَكُونَ
عَلَيْكَ حَرَجٌ ۗ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿٥٠﴾

51. Umuahirishe umtakaye miongoni mwao, na umsogeze umtakaye. Na kama ukimtaka yule uliyemtenga, basi si vibaya kwako. Kufanya hivi kutapelekea yaburudike (yafurahi) macho yao, (ziridhie nyoyo zao) wala wasihuzunike, na wawe radhi juu ya kile unachowapa, wao wote. Na Mwenyezi Mungu Anajua yaliyomo nyoyoni mwenu, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mpole.

تُرْجِي مَنْ تَشَاءُ مِنْهُنَّ وَتُؤْوِي إِلَيْكَ مَنْ تَشَاءُ ۖ
وَمَنِ ابْتَغَيْتَ مِمَّنْ عَزَلْتَ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكَ ۚ
ذَٰلِكَ أَدْنَىٰ أَنْ تَقَرَّ أَعْيُنُهُنَّ وَلَا يَحْزَنَّ وَيَرْضَيْنَ
بِمَا آتَيْتَهُنَّ كُلُّهُنَّ ۚ وَاللَّهُ يَعْلَمُ مَا فِي قُلُوبِكُمْ ۚ
وَكَانَ اللَّهُ عَلِيمًا حَلِيمًا ﴿٥١﴾

52. Baada ya hawa (wake ulio nao), si halali kwako (kuoa) wanawake (wengine, ukazidisha kuliko idadi ya hawa ulio nao); wala (si halali) kuwabadilisha kwa wake wengine (ili idadi iwe ile ile sawa sawa), ingawa uzuri wao (wa mambo yao) utakupendeza; isipokuwa yule uliyemtamalaki kwa mkono wako wa kulia. Na Mwenyezi Mungu ni Mchunguaji (Mtazamaji) wa kila kitu.

لَا يَحِلُّ لَكَ النِّسَاءُ مِنْ بَعْدُ وَلَا أَنْ تَبَدَّلَ بِهِنَّ
مِنْ أَزْوَاجٍ وَلَوْ أَعْجَبَكَ حُسْنُهُنَّ إِلَّا مَا مَلَكَتْ
يَمِينُكَ ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ رَقِيبًا ﴿٥٢﴾ ع

---

49. Ukimuacha mke kabla ya kuingia nyumbani naye, anaweza kuolewa pale pale na mume mwingine, hakai eda kwani hapana matarajio ya kuwa ana mimba ya mume huyo, na inampasa huyo mume aliyemuacha ampe nusu ya mahari aliyomuolea. Na kama huyo mwanamke aliingia khasarani kwa kuvunjika ndoa hiyo kwa kuwa — labda amenunua vitu vingi, basi anaweza kushitaki katika Court, na kadhi au Jaji watatazama cha kumfidia.

51. Mwenyezi Mungu — kwa kuujua mwendo mzuri kabisa wa Mtume usiokuwa na mfano — amenuondoshea wajibati za mume zinazokuwa juu yake juu ya wake zake. Kaondoshewa haya ili waone wenyewe hao wake zake namna gani Mtume anavyokaa nao vizuri hivyo, na hali ya kuwa ameachiwa awafanye atakavyo. Basi seuze sisi tuliofungwa kwa wajibati kubwa kubwa tuwafanyie wake zetu; basi natuwafanyie zote, bali na zaidi kwani ziada ya kheri ni kheri.

53. Enyi mlioamini! Msiingie nyumba za Mtume ila mpewe ruhusa kwenda kula, pasipo (kwenda kukaa) kungojea kiive. Lakini mtakapoitwa ingieni, na mnapokwisha kula tawanyikeni. Wala msiweke mazungumzo, maana jambo hili linamuudhi Mtume, naye anakuoneeni haya; lakini Mwenyezi Mungu Haoni haya kusema haki. Nanyi mnapowauliza (wakeze) waulizeni nyuma ya pazia. Kufanya haya kutasafisha nyoyo zenu na nyoyo zao. Wala haikupasieni (haitakikani) kumuudhi Mtume wa Mwenyezi Mungu. Wala kuwaoa wake zake baada yake; kabisa. Hakika jambo hilo ni (dhambi) kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu.

يا أيها الذين آمنوا لا تدخلوا بيوت النبي إلا
أن يؤذن لكم إلى طعام غير نظرين
إنه ولكن إذا دعيتم فادخلوا فإذا طعمتم
فانتشروا ولا مستأنسين لحديث إن ذلكم كان
يؤذي النبي فيستحي منكم والله لا يستحي من
الحق وإذا سألتموهن متاعا فسئلوهن من وراء
حجاب ذلكم أطهر لقلوبكم وقلوبهن وما كان
لكم أن تؤذوا رسول الله ولا أن تنكحوا أزواجه
من بعده أبدا إن ذلكم كان عند الله عظيما ﴿٥٣﴾

54. Mkidhihirisha chochote kile au kukificha, (Mwenyezi Mungu atajua tu) kwani Mwenyezi Mungu Anajua kila kitu.

إن تبدوا شيئا أو تخفوه فإن الله كان بكل شيء
عليما ﴿٥٤﴾

55. Si dhambi juu yao (wanawake) katika (kuonana na) baba zao, wala watoto wao, wala kaka zao, wala wana wa kaka zao, wala wana wa dada zao, wala wanawake wenziwao, wala wale iliyowatamalaki mikono yao ya kulia. Muogopeni Mwenyezi Mungu (enyi wanawake)! bila shaka Mwenyezi Mungu ni Shahidi juu ya kila kitu.

لا جناح عليهن في آبائهن ولا أبنائهن
ولا إخوانهن ولا أبناء إخوانهن ولا أبناء
أخواتهن ولا نسائهن ولا ما ملكت أيمانهن
واتقين الله إن الله كان على كل شيء شهيدا ﴿٥٥﴾

56. Hakika Mwenyezi Mungu anamteremshia rehema Mtume; na Malaika Wake (wanamuombea dua kwa vile vitendo vizuri alivyovifanya). Basi; enyi Waislamu (mliopata neema hii ya kufundishwa haya na Mtume) msalieni (Mtume, muombeeni rehema) na muombeeni amani.

إن الله وملائكته يصلون على النبي يا أيها الذين
آمنوا صلوا عليه وسلموا تسليما ﴿٥٦﴾

57. Kwa yakini wale wanaomuudhi Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, Mwenyezi Mungu Amewalaani katika dunia na Akhera, na Amewaandalia adhabu ifedheheshayo.

إن الذين يؤذون الله ورسوله لعنهم الله في
الدنيا والآخرة وأعد لهم عذابا مهينا ﴿٥٧﴾

58. Na wale wanaowaudhi wanaume Waislamu na wanawake Waislamu pasipo wao kufanya kosa

والذين يؤذون المؤمنين والمؤمنات بغير

53. Kama wakeze Mtume wangeolewa na watu wengine, isingekuwa sahali kwa watu kwenda pata kwao habari za mambo ya dini waliyojifunza kwa Mtume.

Na wamekatazwa mwanzo wa Aya hii watu kuwa maroho — kwenda majumbani mwa watu wakati wa chakula. Na wakikaribishwa wasiwe wepesi kula. "Karibu" ni mila, "Karibu" si kula. Na wakisha kula wende zao, wapate wenyewe kupumzika . . .

56. Kwa kusema kama hivi: (a) *Allahumma Salli Alaa Muhammadin wa Alaa Ali Muhammad, Kamaa Sallayta Alaa Ibrahima wa Alaa Ali Ibrahim. Wabaarik Alaa Muhammadin wa Alaa Ali Muhammad, kamaa Baarakta Alaa Ibrahima wa Alaa Ali Ibrahim. Wasallim Alaa Muhammadin wa Alaa Ali Muhammad, kamaa Sallamta Alaa Ibrahima wa Alaa Ali Ibrahim Fil Alamin. Innaka Hamydun Majyd;* au (b) *Assalaatu Wassalaamu Alan Nabiyyi Warahmatullahi Wabarakaatuhu;* au (c) *Allahumma Salli Wasallim Wabaarik Alaa Muhammadin wa Alaa Ali Muhammad, Adada Khalqika, Waridhaa Nafsika, Wazinata Arshika, Wamidaada Kalimaatik.*

مَا اكْتَسَبُوا فَقَدِ احْتَمَلُوا بُهْتَانًا وَإِثْمًا مُّبِينًا ﴿٥٨﴾

lolote, bila shaka wamebeba dhulma kubwa na dhambi zilizo dhahiri.

يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ قُل لِّأَزْوَاجِكَ وَبَنَاتِكَ وَنِسَاءِ الْمُؤْمِنِينَ يُدْنِينَ عَلَيْهِنَّ مِن جَلَابِيبِهِنَّ ۚ ذَٰلِكَ أَدْنَىٰ أَن يُعْرَفْنَ فَلَا يُؤْذَيْنَ ۗ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَّحِيمًا ﴿٥٩﴾

59. Ewe Mtume! Waambie wake zako, na binti zako, na wanawake wa Kiislamu (wengine — waambie), wajiteremshie uzuri nguo zao. Kufanya hivyo kutapelekea upesi wajulikane (kuwa ni watu wa hishima ili) wasiudhiwe. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

لَّئِن لَّمْ يَنتَهِ الْمُنَافِقُونَ وَالَّذِينَ فِي قُلُوبِهِم مَّرَضٌ وَالْمُرْجِفُونَ فِي الْمَدِينَةِ لَنُغْرِيَنَّكَ بِهِمْ ثُمَّ لَا يُجَاوِرُونَكَ فِيهَا إِلَّا قَلِيلًا ﴿٦٠﴾

60. Kama wanafiki na wale wenye maradhi nyoyoni mwao na watangazao uovu mjini, hawataacha (visa vyao hivyo vya upotofu), kwa yakini tutakusalitisha (Tutakuondokesha) juu yao, kisha hawatakaa humo karibu yako ila muda kidogo tu; (kisha litawafika la kuwafika).

مَّلْعُونِينَ ۖ أَيْنَمَا ثُقِفُوا أُخِذُوا وَقُتِّلُوا تَقْتِيلًا ﴿٦١﴾

61. Maluuni (hao); popote waonekanapo wakamatwe na wauawe kabisa.

سُنَّةَ اللَّهِ فِي الَّذِينَ خَلَوْا مِن قَبْلُ ۖ وَلَن تَجِدَ لِسُنَّةِ اللَّهِ تَبْدِيلًا ﴿٦٢﴾

62. Hii ni kawaida ya Mwenyezi Mungu iliyokuwa kwa wale waliopita zamani; wala hutapata mabadiliko katika kawaida ya Mwenyezi Mungu.

يَسْأَلُكَ النَّاسُ عَنِ السَّاعَةِ ۖ قُلْ إِنَّمَا عِلْمُهَا عِندَ اللَّهِ ۚ وَمَا يُدْرِيكَ لَعَلَّ السَّاعَةَ تَكُونُ قَرِيبًا ﴿٦٣﴾

63. Watu wanakuuliza habari za Kiama (kitakuja lini). Sema: "Ilimu yake iko kwa Mwenyezi Mungu tu." Na kipi kitakujulisha (lini Kiama). Pengine kiama kiko karibu.

إِنَّ اللَّهَ لَعَنَ الْكَافِرِينَ وَأَعَدَّ لَهُمْ سَعِيرًا ﴿٦٤﴾

64. Kwa hakika Mwenyezi Mungu Amewalaani makafiri na Amewaandalia Moto (unaowaka kweli kweli)

خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ۖ لَّا يَجِدُونَ وَلِيًّا وَلَا نَصِيرًا ﴿٦٥﴾

65. Watakaa humo daima; hawatapata kipenzi wala msaidizi.

يَوْمَ تُقَلَّبُ وُجُوهُهُمْ فِي النَّارِ يَقُولُونَ يَا لَيْتَنَا أَطَعْنَا اللَّهَ وَأَطَعْنَا الرَّسُولَا ﴿٦٦﴾

66. Siku ambayo nyuso zao zitapinduliwa pinduliwa (zitapounguzwa) Motoni, waseme: "Laiti tungemtii Mwenyezi Mungu na tungemtii Mtume."

وَقَالُوا رَبَّنَا إِنَّا أَطَعْنَا سَادَتَنَا وَكُبَرَاءَنَا فَأَضَلُّونَا السَّبِيلَا ﴿٦٧﴾

67. Na watasema: "Mola wetu! Hakika tumewafuata mabwana wetu na wakubwa wetu, basi wao wametupoteza njia."

رَبَّنَا آتِهِمْ ضِعْفَيْنِ مِنَ الْعَذَابِ وَالْعَنْهُمْ لَعْنًا كَبِيرًا ﴿٦٨﴾

68. "Mola wetu! Wape hawa adhabu maradufu (kubwa zaidi) na uwalaani laana kubwa."

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَكُونُوا كَالَّذِينَ آذَوْا مُوسَىٰ فَبَرَّأَهُ اللَّهُ مِمَّا قَالُوا ۚ وَكَانَ عِندَ اللَّهِ وَجِيهًا ﴿٦٩﴾

69. Enyi mlioamini! Msiwe kama wale waliomtaabisha Musa, lakini Mwenyezi Mungu Alimtakasa na yale waliyoyasema, naye alikuwa mwenye hishima mbele ya Mwenyezi Mungu.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَقُولُوا قَوْلًا سَدِيدًا ﴿٧٠﴾

70. Enyi mlioamini! Muogopeni Mwenyezi Mungu na semeni maneno ya haki

71. Atakutengenezeeni vizuri vitendo vyenu na Atakusameheni madhambi yenu; Na anayemtii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, bila shaka amefanikiwa mafanikio makubwa.

يُصْلِحْ لَكُمْ أَعْمَالَكُمْ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ ۗ
وَمَن يُطِعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ فَازَ فَوْزًا عَظِيمًا ﴿٧١﴾

72. Kwa yakini Sisi Tulizidhihirisha amri zetu na makatazo yetu, (tukaziuliza) mbingu na ardhi na milima (kuwa zitachukua madaraka ya kufuata amri hizo na kujiepusha na makatazo hayo ili zipate Pepo zikifuzu, na Moto zikifeli), vikakataa kuichukua (ahadi hiyo) na vikaiogopa, lakini mwanaadamu akaichukua. Bila shaka yeye ni dhalimu mkubwa (wa nafsi yake kwa kuwa amechukua dhamana hii wala haitekelezi), mjinga sana

إِنَّا عَرَضْنَا الْأَمَانَةَ عَلَى السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَ
الْجِبَالِ فَأَبَيْنَ أَن يَحْمِلْنَهَا وَأَشْفَقْنَ مِنْهَا
وَحَمَلَهَا الْإِنسَانُ ۖ إِنَّهُ كَانَ ظَلُومًا جَهُولًا ﴿٧٢﴾

73. Ili Mwenyezi Mungu Awaadhibu wanaume wanafiki na wanawake wanafiki, na wanaume wenye kushirikisha na wanawake wenye kushirikisha, na awasamehe Waislamu wanaume na Waislamu wanawake; na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

لِّيُعَذِّبَ اللَّهُ الْمُنَافِقِينَ وَالْمُنَافِقَاتِ وَالْمُشْرِكِينَ
وَالْمُشْرِكَاتِ وَيَتُوبَ اللَّهُ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ ۗ
وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَّحِيمًا ﴿٧٣﴾ ع

آياتها ٥٤ (٣٤) سُورَةُ سَبَإٍ مَكِّيَّةٌ (٥٨) ركوعاتها ٦

*Ina Aya 54*

## SURAT SABA
*(Imeteremka Makka)*

*Ina Makara 6*

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

ٱلْحَمْدُ لِلَّهِ ٱلَّذِى لَهُۥ مَا فِى ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَمَا فِى ٱلْأَرْضِ وَلَهُ
ٱلْحَمْدُ فِى ٱلْءَاخِرَةِ ۚ وَهُوَ ٱلْحَكِيمُ ٱلْخَبِيرُ (١)

1. Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu ambaye ni Vyake (vyote) vilivyomo mbinguni na ardhini; na Akhera sifa njema ni Zake pia. Naye ni Mwenye hikima, Mwenye ujuzi (wa kila jambo).

يَعْلَمُ مَا يَلِجُ فِى ٱلْأَرْضِ وَمَا يَخْرُجُ مِنْهَا وَمَا يَنزِلُ
مِنَ ٱلسَّمَآءِ وَمَا يَعْرُجُ فِيهَا ۚ وَهُوَ ٱلرَّحِيمُ ٱلْغَفُورُ (٢)

2. Anajua yaingiayo katika ardhi na yatokayo humo na yateremkayo mbinguni na yapandayo humo; naye ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

وَقَالَ ٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ لَا تَأْتِينَا ٱلسَّاعَةُ ۖ قُلْ بَلَىٰ
وَرَبِّى لَتَأْتِيَنَّكُمْ عَٰلِمِ ٱلْغَيْبِ ۖ لَا يَعْزُبُ عَنْهُ
مِثْقَالُ ذَرَّةٍ فِى ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَلَا فِى ٱلْأَرْضِ وَلَآ أَصْغَرُ
مِن ذَٰلِكَ وَلَآ أَكْبَرُ إِلَّا فِى كِتَٰبٍ مُّبِينٍ (٣)

3. Na walisema waliokufuru: "Hakitatujia hicho Kiama" Sema: "Kwa nini?" Kwa haki ya Mola wangu, bila shaka kitakujieni — (Mola) Ajuaye mambo ya siri (yote); hakifichikani Kwake (kitu chochote hata) kilicho na uzito wa mdudu chungu, katika mbingu wala katika ardhi, wala kidogo kuliko hicho wala kikubwa zaidi; ila (vyote hiyo) vimo katika Kitabu (chake) kielezacho (kila jambo).

لِّيَجْزِىَ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ وَعَمِلُوا۟ ٱلصَّٰلِحَٰتِ ۚ أُو۟لَٰٓئِكَ لَهُم
مَّغْفِرَةٌ وَرِزْقٌ كَرِيمٌ (٤)

4. Awalipe wale walioamini na kufanya vitendo vizuri, hao watapata msamaha na riziki yenye hishima.

وَٱلَّذِينَ سَعَوْ فِىٓ ءَايَٰتِنَا مُعَٰجِزِينَ أُو۟لَٰٓئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ
مِّن رِّجْزٍ أَلِيمٌ (٥)

5. Na wale waliojitahidi kuzipinga Aya Zetu wakaona watatushinda watapata adhabu mbaya iumizayo.

وَيَرَى ٱلَّذِينَ أُوتُوا۟ ٱلْعِلْمَ ٱلَّذِىٓ أُنزِلَ إِلَيْكَ
مِن رَّبِّكَ هُوَ ٱلْحَقَّ وَيَهْدِىٓ إِلَىٰ صِرَٰطِ ٱلْعَزِيزِ
ٱلْحَمِيدِ (٦)

6. Na waliopewa ilimu wanafahamu ya kuwa yale yaliyoteremshwa kwako kutoka kwa Mola wako ndiyo haki, nayo huongoa katika njia ya Mwenye nguvu, Asifiwaye.

وَقَالَ ٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ هَلْ نَدُلُّكُمْ عَلَىٰ رَجُلٍ
يُنَبِّئُكُمْ إِذَا مُزِّقْتُمْ كُلَّ مُمَزَّقٍ إِنَّكُمْ لَفِى
خَلْقٍ جَدِيدٍ (٧)

7. Na waliokufuru walisema (kuambiana wenyewe kwa wenyewe kwa stihzai): "Je! Tukujulisheni mtu anayekuambieni ya kwamba mtakapochambuliwa vipande-vipande (makaburini baada ya kufa kwenu) kuwa (mtafufuliwa na) mtakuwa katika umbo jipya?"

---

1. Mwenye hikima maana yake kila analofanya hulifanya kwa sababu maalum, na kama lilifanywa namna nyengine lingeharibika.

8. (Mwenyezi Mungu anasema): "Je! (Wanamuona) Amezua uwongo juu ya Mwenyezi Mungu au amepata wazimu?" Bali wasioiamini Akhera wamo katika adhabu na upotofu wa mbali kabisa.

افترى على الله كذبا أم به جنة ۚ بل الذين
لا يؤمنون بالآخرة في العذاب والضلل البعيد ⑧

9. Je! Hawaoni yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao ya mbingu na ardhi? Kama Tungependa Tungewadidimiza katika ardhi au Tungeangusha juu yao vipande vya mbingu. Bila shaka katika hayo muna mazingatio kwa kila mja mwelekevu.

أفلم يروا إلى ما بين أيديهم وما خلفهم
من السماء والأرض ۚ إن نشأ نخسف بهم الأرض
أو نسقط عليهم كسفا من السماء ۚ إن في ذلك
لآية لكل عبد منيب ⑨

10. Na kwa hakika, Tulimpa Daudi fadhila kubwa kutoka Kwetu. (Tuliyaamrisha majabali yawe yanaitikia dua za Ibada pamoja naye. Tukayaambia):— "Enyi milima! Rejezeni sauti pamoja naye. Na (nyiye) ndege (pia)." Na Tukamlainishia chuma

ولقد آتينا داود منا فضلا ۖ يجبال أوبي معه
والطير ۖ وألنا له الحديد ⑩

11. (Tukamwambia): "Tengeneza (nguo za chuma) pana, na upime vizuri katika kuunganisha; na fanyeni vitendo vizuri; bila shaka Nayaona (yote) mnayoyatenda."

أن اعمل سبغت وقدر في السرد ۖ واعملوا صلحا ۖ
إني بما تعملون بصير ⑪

12. Na kwa Suleimani (Tukautiisha) upepo (uliokwenda) safari yake ya asubuhi (mwendo wa) mwezi mmoja, na safari yake ya jioni (mwendo wa) mwezi mmoja. Na Tukamyayushia chemchem ya shaba. Na katika majini (kulikuwa na) waliofanya kazi mbele yake kwa idhini ya Mola wake. Na kila anayejitenga na amri Yetu miongoni mwao Tunamuonjesha adhabu ya Moto uwakao.

ولسليمن الريح غدوها شهر ورواحها شهر ۖ
وأسلنا له عين القطر ۖ ومن الجن من يعمل بين
يديه بإذن ربه ۖ ومن يزغ منهم عن أمرنا نذقه
من عذاب السعير ⑫

13. Walikuwa wakimfanyia alipendalo, kama ngome na masanamu na mabunguu (madaste) makubwa kama mahodhi, na masufuria makubwa sana yasiyoondolewa mahali pake. (Tukawaambia): "Fanyeni (amali nzuri), enyi watu wa Daudi kwa kushukuru (neema mlizopewa)." Na ni wachache wanaoshukuru katika waja wangu.

يعملون له ما يشاء من محريب وتمثيل وجفان
كالجواب وقدور رسيت ۚ اعملوا آل داود شكرا ۚ
وقليل من عبادي الشكور ⑬

14. Na Tulipomkidhia mauti (alipokufa), hakuna aliyewajulisha mauti yake ila mnyama wa ardhi, (mchwa) aliyekula fimbo yake. Basi ilipoanguka, majini walitambua kama wangalijua siri wasingalikaa katika adhabu hiyo idhalilishayo.

فلما قضينا عليه الموت ما دلهم على موته إلا
دابة الأرض تأكل منسأته ۖ فلما خر تبينت
الجن أن لو كانوا يعلمون الغيب ما لبثوا
في العذاب المهين ⑭

---

14. Nabii Suleimani alipopata Wahyi kuwa karibu atakufa — na kazi ya majenzi bado haijesha — aliona shauri nzuri ajenge nyumba ya vioo, akae juu ya kiti hapo; iwe wale majini wanamuona. Hata akikata roho watadhani yuhai kwa vile alivyokaa. Basi alikaa juu ya kiti, akapachika fimbo mapajani mwake. Akakaa hivyo dahari, mpaka mchwa walipoila ile fimbo ikaanguka ndipo walipotambua hao majini kuwa Nabii Suleimani amekufa zamani. Wametiwa taabuni bure.

Wamegeuza tafsiri na muradi wa maneno yaliyomo katika hii Aya waliyoifanya ya 15. (a) Wamekanusha tena Majini, wamesema muradi wa tamko la Jini ni binaadamu, sio viumbe vyengine. Na tumeureieza ukafiri wao huu

15. Bila shaka yalikuwa mazingatio kwa (watu wa nchi ya) Saba katika maskani yao. Mabustani (ya pande zote) mbili, kulia na kushoto. "Kuleni katika riziki ya Mola wenu, na mumshukuru: Mji mzuri na Mola Mwingi wa msamaha."

لَقَدْ كَانَ لِسَبَإٍ فِي مَسْكَنِهِمْ آيَةٌ ۖ جَنَّتَانِ عَن يَمِينٍ
وَشِمَالٍ ۖ كُلُوا مِن رِّزْقِ رَبِّكُمْ وَاشْكُرُوا لَهُ ۚ بَلْدَةٌ
طَيِّبَةٌ وَرَبٌّ غَفُورٌ ﴿١٥﴾

16. Lakini walipuza (amri za Mwenyezi Mungu); kwa hivyo Tukawapelekea mfuriko mkubwa (wa maji ukagharikisha mashamba hayo) na Tukawabadilishia kwa mabustani yao hayo (mazuri) mabustani mengine (yaliyotungana yote pande) mbili (vile vile; lakini) yenye matunda makali machungu na mivinje na miti kidogo ya kunazi.

فَأَعْرَضُوا فَأَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ سَيْلَ الْعَرِمِ وَبَدَّلْنَاهُم
بِجَنَّتَيْهِمْ جَنَّتَيْنِ ذَوَاتَيْ أُكُلٍ خَمْطٍ وَأَثْلٍ
وَشَيْءٍ مِّن سِدْرٍ قَلِيلٍ ﴿١٦﴾

17. Haya Tuliwalipa kwa sababu ya kukanusha kwao (neema za Mwenyezi Mungu). Nasi Hatumuadhibu ila anayekufuru.

ذَٰلِكَ جَزَيْنَاهُم بِمَا كَفَرُوا ۖ وَهَلْ نُجَازِي إِلَّا الْكَفُورَ ﴿١٧﴾

18. Na baina yao na baina ya miji Tuliyoibariki mengine, Tuliweka miji iliyo dhahiri, na Tukaweka humo (vituo vya) safari, (tukawaambia): "Nendeni humo usiku na mchana kwa amani."

وَجَعَلْنَا بَيْنَهُمْ وَبَيْنَ الْقُرَى الَّتِي بَارَكْنَا فِيهَا
قُرًى ظَاهِرَةً وَقَدَّرْنَا فِيهَا السَّيْرَ ۖ سِيرُوا فِيهَا
لَيَالِيَ وَأَيَّامًا آمِنِينَ ﴿١٨﴾

19. Lakini (walichukia neema hii) wakasema: "Mola wetu! Uweke mwendo mrefu baina ya safari zetu. (Hivi kuwako miji kila mahala tunapopita hakutuonyeshi kuwa tumo safarini)". Na wakajidhulumu nafsi zao. Ndipo Tukawafanya hadithi, (simulizi za watu sasa; wenyewe hawako); na Tukawatawanya mapote mbali mbali; (hawa wakakimbilia nchi hii na wengine wakakimbilia nchi nyingine). Kwa hakika katika hayo yako mazingatio kwa kila anayesubiri anayeshukuru.

فَقَالُوا رَبَّنَا بَاعِدْ بَيْنَ أَسْفَارِنَا وَظَلَمُوا أَنفُسَهُمْ
فَجَعَلْنَاهُمْ أَحَادِيثَ وَمَزَّقْنَاهُمْ كُلَّ مُمَزَّقٍ ۚ
إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ لِّكُلِّ صَبَّارٍ شَكُورٍ ﴿١٩﴾

20. Na bila shaka Iblisi alisadikisha dhana yake juu yao, nao wakamfuata, isipokuwa kundi la waaminio (kweli kweli).

وَلَقَدْ صَدَّقَ عَلَيْهِمْ إِبْلِيسُ ظَنَّهُ فَاتَّبَعُوهُ إِلَّا
فَرِيقًا مِّنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٢٠﴾

21. Na yeye hakuwa na mamlaka yoyote juu yao, ila kwa sababu Tudhihirishe ni nani mwenye kuamini Akhera na nani anayeitilia shaka; na Mola wako ni Mwenye kuhifadhi kila kitu.

وَمَا كَانَ لَهُ عَلَيْهِم مِّن سُلْطَانٍ إِلَّا لِنَعْلَمَ مَن يُؤْمِنُ
بِالْآخِرَةِ مِمَّنْ هُوَ مِنْهَا فِي شَكٍّ ۗ وَرَبُّكَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ
حَفِيظٌ ﴿٢١﴾

22. Sema: "Waiteni mnaowadaia uungu kinyume cha Mwenyezi Mungu; (wakusaidieni;

قُلِ ادْعُوا الَّذِينَ زَعَمْتُم مِّن دُونِ اللَّهِ ۖ لَا يَمْلِكُونَ

---

katika Aya ya 112 ya *Surat Al An-Am*. (b) Wamegeuza tamko la *Minsaatahu* — (Fimbo yake). Wamesema ufalme wake. Na (c) *Daabbatul Ardh* — (Mchwa). Wamesema maana yake mtoto wake dhaifu. *Dhaifu:* hunasibishiwa sifa ya mchwa? Hawawachi, uwongo na ubatani!

19. Watu wa nchi hizo walitakabari kwa hiyo neema kubwa waliyokuwa nayo, basi baada ya myaka waliharibikiwa barabara na wakatawanyika nchi mbali mbali mpaka imekuwa wanatolewa mfano mbaya mpaka leo. Waarabu husema: *Tafarraquu aydy Sabaa* (Wametawanyika mbali mbali kama walivyotawanyika watu wa nchi ya Sabaa). Na kila wasioishukuru neema wakaitunza yatawafika kama haya, na yanaendelea daima kuwafika. Na kila mwenye kupewa neema asiitunze akaiendesha vilivyo humfika yaya haya.

hawawezi kukusaidieni kitu); hawamiliki (hata) uzito wa mdudu chungu mbinguni wala ardhini, wala hawana ushirika (na Mungu) katika hizo (mbingu wala ardhi); wala Yeye hana msaidizi miongoni mwao.

مِثْقَالَ ذَرَّةٍ فِي السَّمٰوٰتِ وَلَا فِي الْأَرْضِ وَمَا لَهُمْ فِيهِمَا مِنْ شِرْكٍ وَمَا لَهُ مِنْهُمْ مِنْ ظَهِيرٍ ﴿٢٢﴾

23. Wala hautafaa uombezi mbele Yake (Mwenyezi Mungu) ila kwa yule aliyempa idhini. Hata inapoondolewa hofu nyoyoni mwao, husema: ' Mola wenu amesema nini? ' (Na wao) huwaambia: ' (Amesema maneno ya) Haki, naye ndiye Aliye juu, Mkubwa."

وَلَا تَنْفَعُ الشَّفَاعَةُ عِنْدَهُ إِلَّا لِمَنْ أَذِنَ لَهُ حَتَّىٰ إِذَا فُزِّعَ عَنْ قُلُوبِهِمْ قَالُوا مَاذَا قَالَ رَبُّكُمْ قَالُوا الْحَقَّ وَهُوَ الْعَلِيُّ الْكَبِيرُ ﴿٢٣﴾

24. Sema: "Ni nani anayekuruzukuni kutoka mbinguni na ardhini?" Waambie: "Mwenyezi Mungu ." Na (waambie): "Bila shaka sisi au nyinyi tuko juu ya uwongofu au katika upotofu (upotevu) uliodhahiri."

قُلْ مَنْ يَرْزُقُكُمْ مِنَ السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضِ قُلِ اللَّهُ وَإِنَّا أَوْ إِيَّاكُمْ لَعَلَىٰ هُدًى أَوْ فِي ضَلَالٍ مُبِينٍ ﴿٢٤﴾

25. Sema: "Hamtaulizwa kwa makosa tuliyofanya (sisi), wala hatutaulizwa kwa yale mnayoyatenda nyinyi."

قُلْ لَا تُسْأَلُونَ عَمَّا أَجْرَمْنَا وَلَا نُسْأَلُ عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿٢٥﴾

26. Sema: "Mola wetu Atatukusanya, kisha Atatuhukumu baina yetu, kwa haki; naye ndiye Hakimu Ajuaye."

قُلْ يَجْمَعُ بَيْنَنَا رَبُّنَا ثُمَّ يَفْتَحُ بَيْنَنَا بِالْحَقِّ وَهُوَ الْفَتَّاحُ الْعَلِيمُ ﴿٢٦﴾

27. Sema: "Nionyesheni wale mliowaunganisha naye (Mwenyezi Mungu) kuwa washirika (wake). Haiwezekani (kuwa na mshirika). Lakini Yeye (peke yake) ndiye Mwenyezi Mungu, Mwenye nguvu, Mwenye hikima."

قُلْ أَرُونِيَ الَّذِينَ أَلْحَقْتُمْ بِهِ شُرَكَاءَ كَلَّا بَلْ هُوَ اللَّهُ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٢٧﴾

28. Na Hatukukutuma (Hatukukuleta) ila kwa watu wote, uwe Mtoaji wa habari nzuri na Muonyaji; lakini watu wengi hawajui (lolote, wanajifuatia tu waliyowakuta nayo wazee wao).

وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا كَافَّةً لِلنَّاسِ بَشِيرًا وَنَذِيرًا وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٢٨﴾

29. Na wanasema: "Lini (itatimia) ahadi hii (ya kuja Kiama) ikiwa mnasema kweli?"

وَيَقُولُونَ مَتَىٰ هَٰذَا الْوَعْدُ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٢٩﴾

30. Sema: "Mnayo miadi (madhubuti) ya (hiyo) siku ambayo hamtaahirika nayo hata saa moja wala hamtaitangulia."

قُلْ لَكُمْ مِيعَادُ يَوْمٍ لَا تَسْتَأْخِرُونَ عَنْهُ سَاعَةً وَلَا تَسْتَقْدِمُونَ ﴿٣٠﴾

---

24. Mtume hakuambiwa awaambie mara moja kuwa "Nyinyi ni wapotofu," lakini aliambiwa awaambie watumie akili zao, watazame anayoyasema yeye na wanayoyasema wao. Wakitumia akili wataona tu kuwa sehemu moja imo katika upotofu, (nao ndio wao); na sehemu moja iko katika uwongofu; (nao ndio Waislamu).

Anafundishwa Muislamu anapotaka kumlingania katika dini mtu asiyekuwa Muislamu, amvute kwa taratibu, kama kumwambia hivi: "Mmoja katika sisi lazima yuko katika uwongofu, na mmoja yuko katika upotofu. Hebu tutazame mnavyosema nyinyi na tunavyosema sisi. Tulinganishe moja moja." Basi aingie kumlinganishia uzuri wa yale ya Kiislamu na uovu wa yale waliyo nayo wao, kwa taratibu taratibu. Yakimwingia kichwani — na si mkaidi — atafuata Inshaloah.

26, 29 na 30. Wanajua kuwa yaliyomo katika Aya hizi — walizozifanya za nambari hizo — yamekhusu Akhera. Wao wanafanya kuwa yamekhusu hapa duniani.

31. Na wakasema wale waliokufuru: "Hatutaiamini Qurani hii kabisa, wala Vile (vitabu) vilivyokuwa kabla yake." Na ungewaona madhalimu watakaposimamishwa mbele ya Mola wao, wakirudishiana maneno wao kwa wao, (ungeona mambo)! Wale wanyonge watawaambia wale waliojiona wakubwa: "Kama si nyinyi bila shaka tungekuwa Waislamu."

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لَن نُّؤْمِنَ بِهَٰذَا الْقُرْآنِ وَلَا بِالَّذِي بَيْنَ يَدَيْهِ ۗ وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ الظَّالِمُونَ مَوْقُوفُونَ عِندَ رَبِّهِمْ يَرْجِعُ بَعْضُهُمْ إِلَىٰ بَعْضٍ الْقَوْلَ يَقُولُ الَّذِينَ اسْتُضْعِفُوا لِلَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا لَوْلَا أَنتُمْ لَكُنَّا مُؤْمِنِينَ ﴿٣١﴾

32. Waseme wale waliojiona wakubwa kuwaambia wale wanyonge: "Oh! Sisi tulikuzuilieni uwongofu baada ya kukufikieni? (Siyo) Bali nyinyi wenyewe mlikuwa waovu."

قَالَ الَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا لِلَّذِينَ اسْتُضْعِفُوا أَنَحْنُ صَدَدْنَاكُمْ عَنِ الْهُدَىٰ بَعْدَ إِذْ جَاءَكُم ۖ بَلْ كُنتُم مُّجْرِمِينَ ﴿٣٢﴾

33. Na wale wanyonge waseme kuwaambia wale waliojiona wakubwa: "Bali (Mlikuwa mkifanya), vitimbi (hila) usiku na mchana (vya kutuzuilia tusiamini); mlipotuamuru tumkufuru Mwenyezi Mungu na tumfanyie washirika." Nao watangicha majuto watakapoiona adhabu; na Tutaweka makongwa shingoni mwa wale waliokufuru; kwani wanalipwa mengine ila yale waliyokuwa wakiyatenda?

وَقَالَ الَّذِينَ اسْتُضْعِفُوا لِلَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا بَلْ مَكْرُ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ إِذْ تَأْمُرُونَنَا أَن نَّكْفُرَ بِاللَّهِ وَنَجْعَلَ لَهُ أَندَادًا ۚ وَأَسَرُّوا النَّدَامَةَ لَمَّا رَأَوُا الْعَذَابَ وَجَعَلْنَا الْأَغْلَالَ فِي أَعْنَاقِ الَّذِينَ كَفَرُوا ۚ هَلْ يُجْزَوْنَ إِلَّا مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٣٣﴾

34. Basi Hatukumtuma (hatukumpeleka) Muonyaji katika mji wowote ule ila wenyeji wake wajipatao walisema: "Bila shaka sisi tunayakataa haya mliyotumwa nayo."

وَمَا أَرْسَلْنَا فِي قَرْيَةٍ مِّن نَّذِيرٍ إِلَّا قَالَ مُتْرَفُوهَا إِنَّا بِمَا أُرْسِلْتُم بِهِ كَافِرُونَ ﴿٣٤﴾

35. Na wakasema: "Sisi tunayo mali nyingi na watoto wengi, wala sisi hatutaadhibiwa."

وَقَالُوا نَحْنُ أَكْثَرُ أَمْوَالًا وَأَوْلَادًا وَمَا نَحْنُ بِمُعَذَّبِينَ ﴿٣٥﴾

36. Sema: "Kwa yakini Mola wangu Humfungulia riziki Amtakaye (Japokuwa ni mtu mbaya) na Humdhikishia (amtakaye japokuwa ni mtu mwema), lakini watu wengi hawajui."

قُلْ إِنَّ رَبِّي يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَن يَشَاءُ وَيَقْدِرُ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٣٦﴾ ع

37. Na si mali zenu wala watoto wenu watakaokukaribisheni Kwetu katika daraja (za Peponi), isipokuwa aliyeamini na kutenda mema. Basi hao watapata ujira mkubwa kabisa kwa yale waliyotenda; nao watakuwa salama katika maghorofa (ya Peponi).

وَمَا أَمْوَالُكُمْ وَلَا أَوْلَادُكُم بِالَّتِي تُقَرِّبُكُمْ عِندَنَا زُلْفَىٰ إِلَّا مَنْ آمَنَ وَعَمِلَ صَالِحًا فَأُولَٰئِكَ لَهُمْ جَزَاءُ الضِّعْفِ بِمَا عَمِلُوا وَهُمْ فِي الْغُرُفَاتِ آمِنُونَ ﴿٣٧﴾

38. Na wale wanaojitahidi kuzipinga Aya Zetu, wakaona watatushinda hao watahudhurishwa adhabuni.

وَالَّذِينَ يَسْعَوْنَ فِي آيَاتِنَا مُعَاجِزِينَ أُولَٰئِكَ فِي الْعَذَابِ مُحْضَرُونَ ﴿٣٨﴾

39. Sema: "Kwa hakika Mola wangu humkunjulia riziki amtakaye katika waja Wake, na Humdhikishia (amtakaye). Na chochote mtakachotoa, basi Yeye Atakilipa; naye ni Mbora wa wanaoruzuku."

قُلْ إِنَّ رَبِّي يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَن يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ وَيَقْدِرُ لَهُ ۚ وَمَا أَنفَقْتُم مِّن شَيْءٍ فَهُوَ يُخْلِفُهُ ۖ وَهُوَ خَيْرُ الرَّازِقِينَ ﴿٣٩﴾

40. Na (wakumbushe) siku Atakayowakusanya wote, kisha Atawaambia Malaika: "Je! Hawa walikuwa wakikuabuduni?"

وَيَوْمَ يَحْشُرُهُمْ جَمِيعًا ثُمَّ يَقُولُ لِلْمَلَائِكَةِ أَهَٰؤُلَاءِ إِيَّاكُمْ كَانُوا يَعْبُدُونَ ﴿٤٠﴾

41. Waseme: "Umeepukana na kila upunguvu! Wewe ndiwe kipenzi chetu, si hao; bali walikuwa wakiwaabudu majini; wengi wao waliwaamini hao (majini)."

قَالُوا سُبْحَانَكَ أَنتَ وَلِيُّنَا مِن دُونِهِم ۚ بَلْ كَانُوا
يَعْبُدُونَ الْجِنَّ ۖ أَكْثَرُهُم بِهِم مُّؤْمِنُونَ ﴿٤١﴾

42. (Basi Mwenyezi Mungu atawaambia) "Hii leo hawataweza baadhi yenu kuwavutia nafuu wenziwao wala kuwaondoshea madhara." Na Tutawaambia wale waliodhulumu (nafsi zao): "Onjeni adhabu ya Moto mliokuwa mkiukadhibisha."

فَالْيَوْمَ لَا يَمْلِكُ بَعْضُكُمْ لِبَعْضٍ نَّفْعًا وَلَا ضَرًّا ۖ
وَنَقُولُ لِلَّذِينَ ظَلَمُوا ذُوقُوا عَذَابَ النَّارِ الَّتِي كُنتُم
بِهَا تُكَذِّبُونَ ﴿٤٢﴾

43. Na wanaposomewa Aya Zetu hizi zilizo wazi kabisa, husema: "Hakuwa huyo (Muhammad) ila ni mtu anayetaka kukuzuieni na (ile ibada) waliyokuwa wakiabudu baba zenu." Na wakasema: "Hayakuwa haya ila ni uwongo uliozuliwa." Na wakasema wale waliokufuru kuiambia haki ilipowajia: "Haukuwa huu ila ni uchawi ulio dhahiri."

وَإِذَا تُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ آيَاتُنَا بَيِّنَاتٍ قَالُوا مَا هَٰذَا إِلَّا رَجُلٌ
يُرِيدُ أَن يَصُدَّكُمْ عَمَّا كَانَ يَعْبُدُ آبَاؤُكُمْ وَقَالُوا
مَا هَٰذَا إِلَّا إِفْكٌ مُّفْتَرًى ۚ وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِلْحَقِّ
لَمَّا جَاءَهُمْ إِنْ هَٰذَا إِلَّا سِحْرٌ مُّبِينٌ ﴿٤٣﴾

44. Wala (hawa Waarabu) Hatukuwapa vitabu (kabla ya kitabu hiki, wakawa) wanavisoma, wala hatukuwapelekea Muonyaji kabla yako. (Basi wamejuaje kuwa huu ni uwongo?)

وَمَا آتَيْنَاهُم مِّن كُتُبٍ يَدْرُسُونَهَا ۖ وَمَا أَرْسَلْنَا
إِلَيْهِمْ قَبْلَكَ مِن نَّذِيرٍ ﴿٤٤﴾

45. Na walikadhibisha wale waliokuwa kabla yao. Na hawajapata (hawa Waarabu hata) sehemu ya kumi ya Tulivyowapa hao; Waliwakadhibisha Mitume Wangu. Basi adhabu Yangu ilikuwa namna gani (kwao)?

وَكَذَّبَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَمَا بَلَغُوا مِعْشَارَ
ع مَا آتَيْنَاهُمْ فَكَذَّبُوا رُسُلِي ۖ فَكَيْفَ كَانَ نَكِيرِ ﴿٤٥﴾

46. Sema: "Mimi nakunasihini kwa jambo moja tu: ya kwamba msimame kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, wawili-wawili na mmoja-mmoja, kisha mfikiri; (Mtaona kuwa huyu Muhammad kila anayoyasema ni haki; na mtaona kuwa) Mwenzenu huyu hana wazimu: hakuwa yeye ila ni Muonyaji wenu kabla ya kufika adhabu kali."

قُلْ إِنَّمَا أَعِظُكُم بِوَاحِدَةٍ ۖ أَن تَقُومُوا لِلَّهِ مَثْنَىٰ
وَفُرَادَىٰ ثُمَّ تَتَفَكَّرُوا ۚ مَا بِصَاحِبِكُم مِّن جِنَّةٍ ۚ
إِنْ هُوَ إِلَّا نَذِيرٌ لَّكُم بَيْنَ يَدَيْ عَذَابٍ شَدِيدٍ ﴿٤٦﴾

47. Sema: "Ujira niliokuombeni (kama nalipata kukuombeni), basi huo ni wenu nyinyi (uchukueni). Hauko ujira wangu ila kwa Mwenyezi Mungu tu, naye ni Shahidi juu ya kila kitu."

قُلْ مَا سَأَلْتُكُم مِّنْ أَجْرٍ فَهُوَ لَكُمْ ۖ إِنْ أَجْرِيَ إِلَّا
عَلَى اللَّهِ ۖ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ ﴿٤٧﴾

48. Sema: "Bila shaka Mola wangu anaitawanya haki, Mjuzi wa (mambo ya) ghaibu."

قُلْ إِنَّ رَبِّي يَقْذِفُ بِالْحَقِّ عَلَّامُ الْغُيُوبِ ﴿٤٨﴾

49. Sema: "(Dini ya) haki imekuja, na (ile dini ya) uwongo (ya masanamu) haitaleta mapya tena wala haitaweza kurejesha (nguvu zake)."

قُلْ جَاءَ الْحَقُّ وَمَا يُبْدِئُ الْبَاطِلُ وَمَا يُعِيدُ ﴿٤٩﴾

---

46. Uislamu hauogopi kupingwa kwa hoja. Kwa hivyo unawataka watu wakae, wafikiri juu ya mambo ya Uislamu, wayepime na yao, wataona kuwa ya Uislamu ndiyo ya haki.

قُلْ إِن ضَلَلْتُ فَإِنَّمَآ أَضِلُّ عَلَىٰ نَفْسِى ۖ وَإِنِ اهْتَدَيْتُ فَبِمَا يُوحِىٓ إِلَىَّ رَبِّىٓ ۚ إِنَّهُۥ سَمِيعٌ قَرِيبٌ ﴿٥٠﴾

50. Sema: "Kama nimepotea, basi nimepotea kwa kudhuru nafsi yangu mwenyewe; na kama nimeongoka, basi ni kwa sababu ya kunileteа Wahyi (kunifunulia) Mola wangu. Bila shaka Yeye ni Mwenye kusikia, Aliye karibu (yetu sote)."

وَلَوْ تَرَىٰٓ إِذْ فَزِعُوا فَلَا فَوْتَ وَأُخِذُوا مِن مَّكَانٍ قَرِيبٍ ﴿٥١﴾

51. Na ungaliona watakapofazaika, (watakapohangaika) (watakapoiona adhabu ya Mwenyezi Mungu), (watake kukimbia); lakini hakuna makimbilio, na watakamatwa (mara moja) mahala pa karibu (kabla hawajafika popote)

وَقَالُوٓا ءَامَنَّا بِهِۦ وَأَنَّىٰ لَهُمُ التَّنَاوُشُ مِن مَّكَانٍۭ بَعِيدٍ ﴿٥٢﴾

52. Na watasema (wakati huo katika kutapatapa kwao) "Tunaiamini (sasa dini ya Uislamu)," lakini watawezaje kuupata (Uislamu huko) mahali pa mbali?

وَقَدْ كَفَرُوا بِهِۦ مِن قَبْلُ ۖ وَيَقْذِفُونَ بِالْغَيْبِ مِن مَّكَانٍۭ بَعِيدٍ ﴿٥٣﴾

53. Na hali ya kuwa walikwisha kuukanusha zamani, na walikuwa wakiyatupilia mbali maneno ya Ghaibu yaliyotoka kwa Mwenyezi Mungu, (waliyatupa mahali pa mbali).

وَحِيلَ بَيْنَهُمْ وَبَيْنَ مَا يَشْتَهُونَ كَمَا فُعِلَ بِأَشْيَاعِهِم مِّن قَبْلُ ۚ إِنَّهُمْ كَانُوا فِى شَكٍّ مُّرِيبٍۭ ﴿٥٤﴾ ع

54. Na watatiliwa kizuizi baina yao na baina ya yale wanayoyatamani, kama walivyofanyiwa wenzao zamani. Bila shaka walikuwa katika shaka iliyowatia tuhuma (juu ya dini ya Uislamu).

آياتها ٤٥ (٣٥) سُورَةُ فَاطِرٍ مَكِّيَّةٌ (٤٣) ركوعاتها ٥

## SURAT FATIR

*Imeteremka Makka*

*Ina Aya 45* *Ina Makara 5*

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

الْحَمْدُ لِلَّهِ فَاطِرِ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ جَاعِلِ الْمَلَائِكَةِ رُسُلًا أُولِي أَجْنِحَةٍ مَثْنَىٰ وَثُلَاثَ وَرُبَاعَ ۚ يَزِيدُ فِي الْخَلْقِ مَا يَشَاءُ ۚ إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ①

1. Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, Muumba wa mbingu na ardhi, aliyewafanya Malaika kuwa wajumbe wenye mbawa, mbili mbili na tatu-tatu, na nne-nne. Huzidisha katika kuumba Apendavyo. Bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu.

مَا يَفْتَحِ اللَّهُ لِلنَّاسِ مِنْ رَحْمَةٍ فَلَا مُمْسِكَ لَهَا ۖ وَمَا يُمْسِكْ فَلَا مُرْسِلَ لَهُ مِنْ بَعْدِهِ ۚ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ②

2. Rehema Anayoifungua Mwenyezi Mungu kwa watu, hakuna wa kuizuia; na Anayoizuia hakuna wa kuipeleka mbele (isipokuwa Atake Atakapotaka). Naye ni Mwenye Nguvu, Mwenye hikima.

يَا أَيُّهَا النَّاسُ اذْكُرُوا نِعْمَتَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ ۚ هَلْ مِنْ خَالِقٍ غَيْرُ اللَّهِ يَرْزُقُكُمْ مِنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ ۚ لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ۖ فَأَنَّىٰ تُؤْفَكُونَ ③

3. Enyi watu! Kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu zilizoko juu yenu. Je, yuko muumba mwingine asiyekuwa Mwenyezi Mungu, anayekupeni riziki kutoka mbinguni na ardhini? Hakuna aabudiwaye kwa haki ila Yeye tu; basi wapi mnakopinduliwa?

وَإِنْ يُكَذِّبُوكَ فَقَدْ كُذِّبَتْ رُسُلٌ مِنْ قَبْلِكَ ۚ وَإِلَى اللَّهِ تُرْجَعُ الْأُمُورُ ④

4. Na kama wanakukadhibisha, wamekwishakadhibishwa Mitume kabla yako, (si ajabu ukikadhibishwa). Na mambo yote yatarudishwa kwa Mwenyezi Mungu.

يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنَّ وَعْدَ اللَّهِ حَقٌّ ۖ فَلَا تَغُرَّنَّكُمُ الْحَيَاةُ الدُّنْيَا ۖ وَلَا يَغُرَّنَّكُمْ بِاللَّهِ الْغَرُورُ ⑤

5. Enyi watu! Bila shaka ahadi ya Mwenyezi Mungu ni haki. Basi yasikudanganyeni maisha ya dunia, wala yule mdanganyaji mkubwa (Iblisi) asikudanganyeni juu ya Mwenyezi Mungu.

إِنَّ الشَّيْطَانَ لَكُمْ عَدُوٌّ فَاتَّخِذُوهُ عَدُوًّا ۚ إِنَّمَا يَدْعُو حِزْبَهُ لِيَكُونُوا مِنْ أَصْحَابِ السَّعِيرِ ⑥

6. Kwa yakini Shetani ni adui yenu, basi mfanyeni adui (yenu; kwa hivyo msimtii) kwani analita (analiita), kundi lake liwe katika watu wa Motoni.

الَّذِينَ كَفَرُوا لَهُمْ عَذَابٌ شَدِيدٌ ۖ وَالَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَهُمْ مَغْفِرَةٌ وَأَجْرٌ كَبِيرٌ ⑦ ع

7. Waliokufuru itakuwa kwao adhabu kali; na wale walioamini na wakatenda mema, wao watapata msamaha na ujira mkubwa.

---

1. Inamkinika kuwa muradi wa Mbawa ni nguvu na uweza. Malaika wamepewa nguvu mbali mbali kwa kiasi cha kazi mbali mbali wanazozifanya. Wengine wana nguvu zaidi kuliko wengine.

8. Je! Yule aliyepambiwa amali zake mbaya na akaziona njema, (utamwambia nini hata asikiye)? Bila shaka Mwenyezi Mungu Humuacha kupotea Amtakaye (kwa kuwa hataki mwenyewe kuongoka); na Humuongoza Amtakaye. Basi roho yako isitoke kwa majonzi juu yao; kwa yakini Mwenyezi Mungu Anayajua (yote) wanayoyafanya.

أَفَمَن زُيِّنَ لَهُۥ سُوٓءُ عَمَلِهِۦ فَرَءَاهُ حَسَنًا ۖ
فَإِنَّ ٱللَّهَ يُضِلُّ مَن يَشَآءُ وَيَهْدِى مَن يَشَآءُ ۖ
فَلَا تَذْهَبْ نَفْسُكَ عَلَيْهِمْ حَسَرَٰتٍ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ عَلِيمٌۢ
بِمَا يَصْنَعُونَ ﴿٨﴾

9. Na Mwenyezi Mungu ndiye Anayepeleka pepo zikaharikisha mawingu na Tutayafikisha katika nchi iliyokufa, na kwayo Tukaihuisha ardhi baada ya kufa kwake. Kama hivyo ndivyo (kutakavyokuwa) kufufuliwa.

وَٱللَّهُ ٱلَّذِىٓ أَرْسَلَ ٱلرِّيَٰحَ فَتُثِيرُ سَحَابًا فَسُقْنَٰهُ
إِلَىٰ بَلَدٍ مَّيِّتٍ فَأَحْيَيْنَا بِهِ ٱلْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا ۚ
كَذَٰلِكَ ٱلنُّشُورُ ﴿٩﴾

10. Anayetaka ukubwa (naamtii Mwenyezi Mungu) kwani ukubwa wote ni wa Mwenyezi Mungu tu. Kwake hupanda maneno mazuri; na kitendo kizuri huyapandisha (hayo maneno mazuri. Maneno mazuri peke yake hayana maana kubwa) Na wale wanaofanya hila ya maovu, hao watapata adhabu kali. Na hila za hao zitaangamia (zitaondoka patupu).

مَن كَانَ يُرِيدُ ٱلْعِزَّةَ فَلِلَّهِ ٱلْعِزَّةُ جَمِيعًا ۚ
إِلَيْهِ يَصْعَدُ ٱلْكَلِمُ ٱلطَّيِّبُ وَٱلْعَمَلُ ٱلصَّٰلِحُ
يَرْفَعُهُۥ ۚ وَٱلَّذِينَ يَمْكُرُونَ ٱلسَّيِّـَٔاتِ لَهُمْ عَذَابٌ
شَدِيدٌ ۖ وَمَكْرُ أُو۟لَٰٓئِكَ هُوَ يَبُورُ ﴿١٠﴾

11. Na Mwenyezi Mungu Amekuumbeni kwa udongo, kisha kwa tone la manii, kisha Akakufanyeni wanaume na wanawake. Na mwanamke yoyote hachukui mimba wala hazai ila kwa ilimu Yake (Mwenyezi Mungu). Na mwenye kupewa umri hapewi umri (zaidi) wala hapunguziwi umri wake ila yamo hayo katika Kitabu (cha Mwenyezi Mungu). Bila shaka (kuyapitisha) haya ni sahali kwa Mwenyezi Mungu.

وَٱللَّهُ خَلَقَكُم مِّن تُرَابٍ ثُمَّ مِن نُّطْفَةٍ ثُمَّ جَعَلَكُمْ
أَزْوَٰجًا ۚ وَمَا تَحْمِلُ مِنْ أُنثَىٰ وَلَا تَضَعُ إِلَّا بِعِلْمِهِۦ ۚ
وَمَا يُعَمَّرُ مِن مُّعَمَّرٍ وَلَا يُنقَصُ مِنْ عُمُرِهِۦٓ إِلَّا فِى
كِتَٰبٍ ۚ إِنَّ ذَٰلِكَ عَلَى ٱللَّهِ يَسِيرٌ ﴿١١﴾

12. Na bahari mbili (hizi: ya maji matamu na chumvi) haziwi sawa; haya ni matamu yenye ladha, kinywaji chake kinateremka uzuri kooni, na haya mengine ni chumvi yenye uchungu; na katika zote mnakula nyama mpya (samaki) na mnatoa mapambo mnayoyavaa (lulu); na ndani yake unaziona marikebu zinakata (maji) ili mpate fadhila Yake na ili mpate kushukuru.

وَمَا يَسْتَوِى ٱلْبَحْرَانِ هَٰذَا عَذْبٌ فُرَاتٌ سَآئِغٌ
شَرَابُهُۥ وَهَٰذَا مِلْحٌ أُجَاجٌ ۖ وَمِن كُلٍّ تَأْكُلُونَ لَحْمًا
طَرِيًّا وَتَسْتَخْرِجُونَ حِلْيَةً تَلْبَسُونَهَا ۖ وَتَرَى ٱلْفُلْكَ
فِيهِ مَوَاخِرَ لِتَبْتَغُوا۟ مِن فَضْلِهِۦ وَلَعَلَّكُمْ
تَشْكُرُونَ ﴿١٢﴾

13. Anauingiza usiku katika mchana na kuuingiza mchana katika usiku, na Amevitiisha jua na mwezi; vyote (vinakwenda mchana na usiku) mpaka muda maalumu ufike. Huyo ndiye Mwenyezi Mungu, Mola wenu, Mwenye Ufalme; na wale mnaowaabudu kinyume Chake, wao hawamiliki hata utando (ugozi) wa kokwa ya tende!

يُولِجُ ٱلَّيْلَ فِى ٱلنَّهَارِ وَيُولِجُ ٱلنَّهَارَ فِى ٱلَّيْلِ وَ
سَخَّرَ ٱلشَّمْسَ وَٱلْقَمَرَ كُلٌّ يَجْرِى لِأَجَلٍ مُّسَمًّى ۚ
ذَٰلِكُمُ ٱللَّهُ رَبُّكُمْ لَهُ ٱلْمُلْكُ ۚ وَٱلَّذِينَ تَدْعُونَ
مِن دُونِهِۦ مَا يَمْلِكُونَ مِن قِطْمِيرٍ ﴿١٣﴾

14. Kama mkiwaomba (masanamu hao), hawasikii wito wenu; na hata kama wakisikia

إِن تَدْعُوهُمْ لَا يَسْمَعُوا۟ دُعَآءَكُمْ ۖ وَلَوْ سَمِعُوا۟ مَا

اسْتَجَابُوا لَكُمْ ۚ وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ يَكْفُرُونَ
بِشِرْكِكُمْ ۚ وَلَا يُنَبِّئُكَ مِثْلُ خَبِيرٍ ﴿١٤﴾

hawatakujibuni (kwani hawana uweza wo wote); na siku ya Kiama watakataa ushirikina wenu. Wala (yoyote) hatakuambia kama (Aambiavyo Mungu) — Mjuzi wa kweli kweli.

يَا أَيُّهَا النَّاسُ أَنْتُمُ الْفُقَرَاءُ إِلَى اللَّهِ ۖ وَاللَّهُ
هُوَ الْغَنِيُّ الْحَمِيدُ ﴿١٥﴾

15. Enyi watu! Nyinyi ndio wenye haja kwa Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu Mkwasi (na nyinyi — hakuhitajieni), Asifiwaye (kwa neema zake juu ya viumbe vyake vyote).

إِنْ يَشَأْ يُذْهِبْكُمْ وَيَأْتِ بِخَلْقٍ جَدِيدٍ ﴿١٦﴾

16. Kama Akitaka Atakuondoeni na Ataleta viumbe wapya.

وَمَا ذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ بِعَزِيزٍ ﴿١٧﴾

17. Na jambo hili si gumu kwa Mwenyezi Mungu.

وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِزْرَ أُخْرَىٰ ۚ وَإِنْ تَدْعُ مُثْقَلَةٌ
إِلَىٰ حِمْلِهَا لَا يُحْمَلْ مِنْهُ شَيْءٌ وَلَوْ كَانَ ذَا قُرْبَىٰ ۗ
إِنَّمَا تُنْذِرُ الَّذِينَ يَخْشَوْنَ رَبَّهُمْ بِالْغَيْبِ وَأَقَامُوا
الصَّلَاةَ ۚ وَمَنْ تَزَكَّىٰ فَإِنَّمَا يَتَزَكَّىٰ لِنَفْسِهِ ۚ وَإِلَى
اللَّهِ الْمَصِيرُ ﴿١٨﴾

18. Wala hatabeba mbebaji mzigo wa mwingine. (Kila mtu atachukua jukumu ya dhambi zake mwenyewe). Na kama aliyetopewa na mzigo wake akimwita (mwingine) kwa ajili ya mzigo wake (amchukuiie) hautachukuliwa hata kidogo (na mtu huyo) ingawa ni jamaa yake. Hakika unawaonya (wakaonyeka) wale tu wanaomuogopa Mola wao, na hali ya kuwa Hawamuoni, na wanasimamisha Sala. Na anayejitakasa, basi anajitakasa kwa ajili ya nafsi yake. Na marejeo (ya viumbe vyote) ni kwa Mwenyezi Mungu.

وَمَا يَسْتَوِي الْأَعْمَىٰ وَالْبَصِيرُ ﴿١٩﴾
وَلَا الظُّلُمَاتُ وَلَا النُّورُ ﴿٢٠﴾
وَلَا الظِّلُّ وَلَا الْحَرُورُ ﴿٢١﴾
وَمَا يَسْتَوِي الْأَحْيَاءُ وَلَا الْأَمْوَاتُ ۚ إِنَّ اللَّهَ يُسْمِعُ
مَنْ يَشَاءُ ۖ وَمَا أَنْتَ بِمُسْمِعٍ مَنْ فِي الْقُبُورِ ﴿٢٢﴾

19. Na kipofu na mwenye macho hawawi sawa

20. Wala giza na nuru

21. Wala kivuli na joto

22. Wala hawawi sawa walio hai na wafu. Kwa yakini Mwenyezi Mungu Humsikilizisha Amtakaye; na wewe huwezi kuwasikilizisha waliomo makaburini. (Na hao kama wamekufa, wamo makaburini).

إِنْ أَنْتَ إِلَّا نَذِيرٌ ﴿٢٣﴾

23. Hukuwa Wewe ila ni muonyaji tu.

إِنَّا أَرْسَلْنَاكَ بِالْحَقِّ بَشِيرًا وَنَذِيرًا ۚ وَإِنْ مِنْ أُمَّةٍ
إِلَّا خَلَا فِيهَا نَذِيرٌ ﴿٢٤﴾

24. Bila shaka Sisi Tumekutuma (Tumekuleta) kwa haki ili ubashiri na uonye. Na hakuna taifa lolote ila alipita humo Muonyaji (Mtume kuwaonya).

وَإِنْ يُكَذِّبُوكَ فَقَدْ كَذَّبَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ
جَاءَتْهُمْ رُسُلُهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ وَبِالزُّبُرِ وَبِالْكِتَابِ الْمُنِيرِ ﴿٢٥﴾

25. Na kama wanakukadhibisha, basi walikwisha kadhibisha wale wa kabla yao. Mitume wao waliwajia kwa dalili wazi wazi na kwa madaftari na kwa Vitabu Vyenye nuru. (Wakakadhibisha).

ثُمَّ أَخَذْتُ الَّذِينَ كَفَرُوا ۖ فَكَيْفَ كَانَ نَكِيرِ ﴿٢٦﴾

26. Kisha Niliwakamata (niliwatia mkononi) wale waliokufuru; basi adhabu Yangu ilikuwa (kali) namna gani!

27. Je! Huoni kwamba Mwenyezi Mungu ameteremsha maji toka mawinguni! Na kwayo Tumeyatoa matunda yenye rangi mbali mbali. Na katika milima imo mistari myeupe na myekundu yenye rangi mbali mbali, na (mengine) myeusi sana.

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ أَنزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَخْرَجْنَا بِهِ
ثَمَرَاتٍ مُّخْتَلِفًا أَلْوَانُهَا ۚ وَمِنَ الْجِبَالِ جُدَدٌ
بِيضٌ وَحُمْرٌ مُّخْتَلِفٌ أَلْوَانُهَا وَغَرَابِيبُ سُودٌ ﴿٢٧﴾

28. Na katika watu na wanyama wanaotambaa na wanyama (wengine), pia rangi zao ni mbali mbali. Kwa hakika wanaomwogopa Mwenyezi Mungu miongoni mwa waja Wake ni wale wataalamu (wanavyuoni). Bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Msamehevu.

وَمِنَ النَّاسِ وَالدَّوَابِّ وَالْأَنْعَامِ مُخْتَلِفٌ أَلْوَانُهُ
كَذَٰلِكَ ۗ إِنَّمَا يَخْشَى اللَّهَ مِنْ عِبَادِهِ الْعُلَمَاءُ ۗ
إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ غَفُورٌ ﴿٢٨﴾

29. Kwa yakini wale wanaosoma Kitabu cha Mwenyezi Mungu, na wakasimamisha Sala, na katika yale Tuliyowapa wakatoa, kwa siri na kwa dhahiri, hao wanatumai (faida ya) biashara isiyododa (isiyobwaga)

إِنَّ الَّذِينَ يَتْلُونَ كِتَابَ اللَّهِ وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَ
أَنفَقُوا مِمَّا رَزَقْنَاهُمْ سِرًّا وَعَلَانِيَةً يَرْجُونَ
تِجَارَةً لَّن تَبُورَ ﴿٢٩﴾

30. Ili Awape ujira wao kamili na kuwazidishia fadhila Zake. Hakika Yeye ni Mwingi wa msamaha (na) Mwenye shukrani.

لِيُوَفِّيَهُمْ أُجُورَهُمْ وَيَزِيدَهُم مِّن فَضْلِهِ ۚ إِنَّهُ
غَفُورٌ شَكُورٌ ﴿٣٠﴾

31. Na Kitabu Tulichokuletea kwa Wahyi (Tulichokufunulia) ndicho cha haki; kinasadikisha (vitabu) vilivyokuwa kabla yake. Bila shaka Mwenyezi Mungu kwa waja Wake ni Mwenye kuwajua (vyema) na kuwaona (vizuri).

وَالَّذِي أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ مِنَ الْكِتَابِ هُوَ الْحَقُّ
مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ بِعِبَادِهِ لَخَبِيرٌ
بَصِيرٌ ﴿٣١﴾

32. Kisha Tumewarithisha, (tumewapa) Kitabu (hiki cha Qurani) wale Tuliowachagua miongoni mwa waja wetu. Basi wako miongoni mwao wanaodhulumu nafsi zao (kwa kuwa na maasia mengi kuliko mema). Na wako wa kati na kati, (wana mema na mabaya sawa sawa). Na wako wanaokwenda mbele kabisa katika mambo ya kheri, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo fadhila kubwa.

ثُمَّ أَوْرَثْنَا الْكِتَابَ الَّذِينَ اصْطَفَيْنَا مِنْ عِبَادِنَا ۖ
فَمِنْهُمْ ظَالِمٌ لِّنَفْسِهِ وَمِنْهُم مُّقْتَصِدٌ وَمِنْهُمْ
سَابِقٌ بِالْخَيْرَاتِ بِإِذْنِ اللَّهِ ۚ ذَٰلِكَ هُوَ الْفَضْلُ
الْكَبِيرُ ﴿٣٢﴾

33. Mabustani ya milele watayaingia, humo watapambwa vikuku vya dhahabu, na lulu, na nguo zao humo zitakuwa za hariri.

جَنَّاتُ عَدْنٍ يَدْخُلُونَهَا يُحَلَّوْنَ فِيهَا مِنْ
أَسَاوِرَ مِن ذَهَبٍ وَلُؤْلُؤًا ۖ وَلِبَاسُهُمْ فِيهَا حَرِيرٌ ﴿٣٣﴾

---

18. Rejea maelezo ya Aya ya 15 ya bani Israil.

28. Wenye kusoma kweli kweli wakaona namna gani alivyoumba Mwenyezi Mungu na Mashangazo na Hikima zilizomo katika kuumba huko, hao ndio wanaojua kweli ukubwa wa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu hakutuamrisha kusoma ilimu za Fiqhi tu, bali kusoma pia mailimu haya yanayosomeshwa katika Maskuli na Maakedemy na Macollege na Mauniversity na Malaboratory na mwinginepo. Mafunzo yote haya yalikuwa kwa Waislamu; khalafu wameyatupa kama walivyotupa mwendo wao mzuri, basi kila kitu kikawatupa. Na sasa wanaanza kuyarejelea tena, basi na kila ukubwa wao utawarejelea. Hapana kinachompeleka mtu mbele wala kuupeleka uma mbele kuliko ilimu.

32. Katika Aya hii waliyoifanya kuwa ni ya 33 wamepindua muradi wa tamko la "*Dhalimun Linafsihiy.*" Hao ni watu wabaya wanazidhulumu nafsi zao kwa kufanya mabaya. Wao wanasema hao ni watu wazuri, wanaojinyima matamanio ya nafsi zao. Wakiwafasiri hawa "*Dhaalimun Linafsihi*" kuwa ndio wazuri, wale *Saabiqun Bil Khayrat* (waliotajwa hapo pia) watakuwa nani? Hawaachi!

34. Na watasema (katika kushukuru kwao) "Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu Aliyetuondolea huzuni, kwa yakini Mola wetu ni Mwingi wa msamaha (na) Mwenye shukurani."

وَقَالُوا الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي أَذْهَبَ عَنَّا الْحَزَنَ ۖ إِنَّ رَبَّنَا لَغَفُورٌ شَكُورٌ ﴿٣٤﴾

35. "Ambaye kwa fadhila Zake Ametuweka katika nyumba ya kukaa daima; humo haitugusi taabu wala humo hakutugusi kuchoka."

الَّذِي أَحَلَّنَا دَارَ الْمُقَامَةِ مِنْ فَضْلِهِ لَا يَمَسُّنَا فِيهَا نَصَبٌ وَلَا يَمَسُّنَا فِيهَا لُغُوبٌ ﴿٣٥﴾

36. Na wale waliokufuru watakuwa na moto wa Jahanamu, hawatahukumiwa kufa, wala hawatapunguziwa adhabu yake. Hivi ndivyo tunavyomlipa kila asiye na shukurani.

وَالَّذِينَ كَفَرُوا لَهُمْ نَارُ جَهَنَّمَ لَا يُقْضَىٰ عَلَيْهِمْ فَيَمُوتُوا وَلَا يُخَفَّفُ عَنْهُمْ مِنْ عَذَابِهَا ۚ كَذَٰلِكَ نَجْزِي كُلَّ كَفُورٍ ﴿٣٦﴾

37. Nao humo watapiga makelele, (watalia wanasema): "Mola wetu! Tutoe (Motoni uturejeze duniani), tutafanya vitendo vizuri visivyokuwa vile tulivyokuwa tukifanya." (Mwenyezi Mungu awaambie): "Hatukukupeni umri wa (kuweza) kukumbuka mwenye kukumbuka? Na akakujieni Muonyaji. Basi onjeni (adhabu) madhalimu hawana wa kuwanusuru."

وَهُمْ يَصْطَرِخُونَ فِيهَا رَبَّنَا أَخْرِجْنَا نَعْمَلْ صَالِحًا غَيْرَ الَّذِي كُنَّا نَعْمَلُ ۚ أَوَلَمْ نُعَمِّرْكُمْ مَا يَتَذَكَّرُ فِيهِ مَنْ تَذَكَّرَ وَجَاءَكُمُ النَّذِيرُ ۖ فَذُوقُوا فَمَا لِلظَّالِمِينَ مِنْ نَصِيرٍ ﴿٣٧﴾

38. Kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa siri za mbinguni na ardhini; bila shaka Yeye ni Mjuzi wa yaliyomo vifuani, (seuze yaliyo nje).

إِنَّ اللَّهَ عَالِمُ غَيْبِ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ ۚ إِنَّهُ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿٣٨﴾

39. Yeye ndiye Aliyekufanyeni manaibu katika ardhi (hii; wakifa hawa wanazaliwa hawa). Na anayekufuru, basi (madhara ya) kufuru yake ni juu yake; na kufuru za makafiri haziwazidishii mbele ya Mola wao ila kuchukiwa, wala kufuru za makafiri haziwazidishii ila hasara.

هُوَ الَّذِي جَعَلَكُمْ خَلَائِفَ فِي الْأَرْضِ ۚ فَمَنْ كَفَرَ فَعَلَيْهِ كُفْرُهُ ۖ وَلَا يَزِيدُ الْكَافِرِينَ كُفْرُهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ إِلَّا مَقْتًا ۖ وَلَا يَزِيدُ الْكَافِرِينَ كُفْرُهُمْ إِلَّا خَسَارًا ﴿٣٩﴾

40. Sema: "Mnawaona washirika wenu (hawa mnaowashirikisha na Mwenyezi Mungu) mnaowaabudu wao badala ya Mwenyezi Mungu? Nionyesheni ni sehemu ipi ya ardhi waliyoiumba; au wanayo shirika katika mbingu?" Au tumewapa (hawa makafiri) Kitabu (kabla ya hii Qurani); nao kwa hicho wakawa na dalili waziwazi (ya kuwakubalishia ukafiri wao)? Lakini madhalimu hawa hawaahidiani wao kwa wao ila udanganyifu tu (kudanganyana).

قُلْ أَرَأَيْتُمْ شُرَكَاءَكُمُ الَّذِينَ تَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ أَرُونِي مَاذَا خَلَقُوا مِنَ الْأَرْضِ أَمْ لَهُمْ شِرْكٌ فِي السَّمَاوَاتِ أَمْ آتَيْنَاهُمْ كِتَابًا فَهُمْ عَلَىٰ بَيِّنَتٍ مِنْهُ ۚ بَلْ إِنْ يَعِدُ الظَّالِمُونَ بَعْضُهُمْ بَعْضًا إِلَّا غُرُورًا ﴿٤٠﴾

41. Kwa yakini Mwenyezi Mungu ndiye anayezuilia mbingu na ardhi zisiondoke, na kama zikiondoka hakuna yoyote wa kuzizuia isipokuwa yeye. Bila shaka yeye ni Mpole, Mwingi wa kusamehe.

إِنَّ اللَّهَ يُمْسِكُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ أَنْ تَزُولَا ۚ وَلَئِنْ زَالَتَا إِنْ أَمْسَكَهُمَا مِنْ أَحَدٍ مِنْ بَعْدِهِ ۚ إِنَّهُ كَانَ حَلِيمًا غَفُورًا ﴿٤١﴾

42. Na (hawa makafiri hapo zamani) waliapa kwa Mwenyezi Mungu kiapo chao kilicho kikubwa wakasema: "Akiwajia Muonyaji, bila shaka watakuwa waongofu zaidi kuliko taifa jingine

وَأَقْسَمُوا بِاللَّهِ جَهْدَ أَيْمَانِهِمْ لَئِنْ جَاءَهُمْ نَذِيرٌ لَيَكُونُنَّ أَهْدَىٰ مِنْ إِحْدَى الْأُمَمِ ۖ فَلَمَّا جَاءَهُمْ نَذِيرٌ

lolote." Lakini alipowajia Muonyaji, hakuwazidishia ila kuikataa (hiyo haki)

43. Kwa ajili ya kutakabari kwao katika ardhi, na kufanya vitimbi vibaya vibaya; na vitimbi vibaya havimteremkii ila yule aliyevifanya. Basi hawangoji ila dasturi (ya Mungu) iliyokuwa, (aliyoipitisha) kwa watu wa zamani! Wala hutapata mabadiliko katika kawaida (dasturi) ya Mwenyezi Mungu (aliyoiweka) wala hutakuta mageuko katika kawaida ya Mwenyezi Mungu.

44. Je! Hawakusafiri katika ardhi wakaona jinsi ulivyokuwa mwisho wa wale waliokuwa kabla yao, na walikuwa wenye nguvu zaidi kuliko wao? Na hakuna kitu kinachoweza kumshinda Mwenyezi Mungu mbinguni wala katika ardhi. Bila shaka yeye ni Mwenye kujua, Mwenye uweza.

45. Na kama Mwenyezi Mungu angaliwatesa watu kwa sababu ya yale waliyoyachuma, asingaliacha juu ya ardhi hata mnyama mmoja. Lakini yeye anawaakhirisha mpaka (ufike huo) muda (maalumu) uliowekwa. Basi itakapokuja ajali yao, (hapo bila shaka watalipwa); na Mwenyezi Mungu anawajua vyema waja wake.

مَّا زَادَهُمْ إِلَّا نُفُورًا (٤٢)

اسْتِكْبَارًا فِي الْأَرْضِ وَمَكْرَ السَّيِّئِ ۚ وَلَا يَحِيقُ الْمَكْرُ
السَّيِّئُ إِلَّا بِأَهْلِهِ ۚ فَهَلْ يَنظُرُونَ إِلَّا سُنَّتَ الْأَوَّلِينَ ۚ
فَلَن تَجِدَ لِسُنَّتِ اللَّهِ تَبْدِيلًا ۖ وَلَن تَجِدَ لِسُنَّتِ اللَّهِ
تَحْوِيلًا (٤٣)

أَوَلَمْ يَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَيَنظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ
الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَكَانُوا أَشَدَّ مِنْهُمْ قُوَّةً ۚ وَمَا كَانَ
اللَّهُ لِيُعْجِزَهُ مِن شَيْءٍ فِي السَّمَاوَاتِ وَلَا فِي الْأَرْضِ ۚ
إِنَّهُ كَانَ عَلِيمًا قَدِيرًا (٤٤)

وَلَوْ يُؤَاخِذُ اللَّهُ النَّاسَ بِمَا كَسَبُوا مَا تَرَكَ عَلَىٰ
ظَهْرِهَا مِن دَابَّةٍ وَلَٰكِن يُؤَخِّرُهُمْ إِلَىٰ أَجَلٍ
مُّسَمًّى ۖ فَإِذَا جَاءَ أَجَلُهُمْ فَإِنَّ اللَّهَ كَانَ
بِعِبَادِهِ بَصِيرًا (٤٥)

اٰيَاتُهَا ٨٣ (٣٦) سُوْرَةُ يٰسٓ مَكِّيَّةٌ (٤١) رُكُوْعَاتُهَا ٥

*Ina Aya 83* *Ina Makaro 5*

## SURATU YA-SIN
*(Imeteremka Makka)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

1. Yaa Syn.

يٰسٓ ۝١

2. Naapa kwa (hii) Qurani yenye kutengenezwa vizuri.

وَالْقُرْاٰنِ الْحَكِيْمِ ۝٢

3. Kuwa hakika wewe ni miongoni mwa Mitume (wa Mwenyezi Mungu)

اِنَّكَ لَمِنَ الْمُرْسَلِيْنَ ۝٣

4. (Na uko) juu ya njia iliyonyoka.

عَلٰى صِرَاطٍ مُّسْتَقِيْمٍ ۝٤

5. (Na hii Qurani) ni uteremsho wa Mwenye nguvu (na) Mwingi wa rehema.

تَنْزِيْلَ الْعَزِيْزِ الرَّحِيْمِ ۝٥

6. Ili uwaonye watu ambao hawakuonywa baba zao (wazee wao); basi wao wamekuwa wenye kughafilika.

لِتُنْذِرَ قَوْمًا مَّآ اُنْذِرَ اٰبَآؤُهُمْ فَهُمْ غٰفِلُوْنَ ۝٦

7. Bila shaka kauli (ya adhabu) imehakikika (imethubutu) juu ya wengi katika wao; kwa hivyo hawaamini.

لَقَدْ حَقَّ الْقَوْلُ عَلٰٓى اَكْثَرِهِمْ فَهُمْ لَا يُؤْمِنُوْنَ ۝٧

8. (Hawa makafiri Hawatazami huku wala huku, wakajua ukweli wa mambo; kama kwamba)

اِنَّا جَعَلْنَا فِيْٓ اَعْنَاقِهِمْ اَغْلٰلًا

---

1. Watu wanaifanyaia vishindo sana Sura hii. Wakaitupa Qurani yote nzima kwa ajili yake. Badala ya kuisoma Qurani kidogo kidogo—kwa makara makara au kwa juzuu juzuu au kwa namna nyingineo yoyote ile — wao wanatoshelezeka na haya kwa kusoma Sura ya *Yaasyn* tu dom daima, asubuhi na jioni. Na haya Mtume ameyakataza. Ameyaamrisha yale ya kusoma Qurani nzima kidogo kidogo tangu juzuu ya *Alif Lam* mpaka juzuu ya *Amma.* Na kila akisha aanze tena. Na akitaka kuzisoma hizo Sura makhsusi azisome baada ya kumaliza hicho kipande cha siku ile cha kusoma Qurani nzima. Ziko Sura makhsusi wanazozifanyia shauku kuzisoma kwa kuwa Sura hizo zimesifiwa kwa sifa makhsusi kwa Hadithi za Mtume. Na wanayoishughulikia zaidi bila kiasi ni hii Sura ya *Yaasyn;* na wakaitolea chungu ya Hadithi za Mtume — kama wanavyozitolea Hadithi hizo Sura zao nyingine. Na nyingi katika hizo ni dhaifu na za uwongo. Kwa hivyo nyingi kabisa katika hizo hazimo katika vile vitabu vinavyotaja Hadithi zilizo sahihi madhubuti, kama vitabu vya: Imam Malik, Al Bukhary, Muslim, Attirmidhy, Abu Daud na An Nasai. Kama hii *Yaasyn,* hadithi yake iliyo bora kabisa katika kutaja fadhila zake ni Hadithi ya Attirmidhy inayosema kuwa:— "Kila kitu kina moyo wake, na moyo wa Qurani ni *Yaasyn.* Atakayesoma mara moja Mwenyezi Mungu atamuandikia thawabu za kama kwamba ameisoma Qurani yote nzima mara kumi." Hadithi hii huyu mwenyewe Attirmidhy papo hapo alipoitaja alisema kuwa ni Hadithi ngeni yaani dhaifu. Basi seuze hizo nyingine. Na hiyo Hadithi inayosema *Yaasyn Limaa Quriat Lahuu* (Kuisoma *Yaasyn* kunampa huyo msomaji hilo alilokusudia), ndiyo kabisa haina nguvu hata chembe wala tamko hili si la Mtume. Yamebainishwa haya katika *Al Maqasidil Hasanah* na *Tamyizut Tayyib Minal Khabyth* na *Asnal Mataalib* na Alluuluul Masnuu na vyinginevyo.

8. Kongwa ni Kongomero linalotiwa katika shingo ya mkhalifu.

فَهِيَ إِلَى الْأَذْقَانِ فَهُمْ مُقْمَحُونَ ⑧

Tumeweka makongwa shingoni mwao, yakawafika videvuni; (hawawezi kugeuka); kwa hivyo vichwa vyao vimeinuliwa.

وَجَعَلْنَا مِنْ بَيْنِ أَيْدِيهِمْ سَدًّا وَمِنْ خَلْفِهِمْ سَدًّا فَأَغْشَيْنَاهُمْ فَهُمْ لَا يُبْصِرُونَ ⑨

9. Na (kama kwamba) Tumeweka kizuwizi mbele yao na kizuwizi nyuma yao na Tumewafunika (macho yao); kwa hivyo hawaoni.

وَسَوَاءٌ عَلَيْهِمْ أَأَنْذَرْتَهُمْ أَمْ لَمْ تُنْذِرْهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ⑩

10. Ni sawa kwao ukiwaonya au usiwaonye, hawataamini.

إِنَّمَا تُنْذِرُ مَنِ اتَّبَعَ الذِّكْرَ وَخَشِيَ الرَّحْمَٰنَ بِالْغَيْبِ فَبَشِّرْهُ بِمَغْفِرَةٍ وَأَجْرٍ كَرِيمٍ ⑪

11. Unaweza kumuonya (akaonyeka) yule anayefuata mauidha na akamwogopa Mwingi wa rehema japo kuwa hamwoni; basi mbashirie huyo (kupata) msamaha na ujira wenye hishima.

إِنَّا نَحْنُ نُحْيِي الْمَوْتَىٰ وَنَكْتُبُ مَا قَدَّمُوا وَآثَارَهُمْ وَكُلَّ شَيْءٍ أَحْصَيْنَاهُ فِي إِمَامٍ مُبِينٍ ⑫

12. Kwa yakini Sisi Tutawahuisha wafu, na Tunaziandika (amali zao wanazozifanya zisiwache) taathira nyuma) na (zile wanazozifanya zikawacha) taathira zao (nyuma). Na kila kitu Tumekihifadhi katika daftari (letu) linalobainisha (kila kitu).

وَاضْرِبْ لَهُمْ مَثَلًا أَصْحَابَ الْقَرْيَةِ إِذْ جَاءَهَا الْمُرْسَلُونَ ⑬

13. Na wapigie mfano (wa) wakazi wa mji mmoja hivi, wajumbe wa dini walipoujia.

إِذْ أَرْسَلْنَا إِلَيْهِمُ اثْنَيْنِ فَكَذَّبُوهُمَا فَعَزَّزْنَا بِثَالِثٍ فَقَالُوا إِنَّا إِلَيْكُمْ مُرْسَلُونَ ⑭

14. Tulipowapelekea (wajumbe) wawili, wakawakadhibisha; basi Tukawazidishia nguvu kwa (mjumbe) wa tatu; wakawaambia: "Kwa yakini sisi tumetumwa kwenu."

قَالُوا مَا أَنْتُمْ إِلَّا بَشَرٌ مِثْلُنَا وَمَا أَنْزَلَ الرَّحْمَٰنُ مِنْ شَيْءٍ إِنْ أَنْتُمْ إِلَّا تَكْذِبُونَ ⑮

15. Wakasema: "Nyinyi si chochote ila ni watu kama sisi, wala (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa rehema hakuteremsha chochote; nyinyi mnasema uwongo tu."

قَالُوا رَبُّنَا يَعْلَمُ إِنَّا إِلَيْكُمْ لَمُرْسَلُونَ ⑯

16. Wakasema: "Mola wetu Anajua bila shaka kuwa sisi tumetumwa kwenu."

وَمَا عَلَيْنَا إِلَّا الْبَلَاغُ الْمُبِينُ ⑰

17. "Wala hapana juu yetu ila kufikisha (ujumbe wetu) waziwazi."

قَالُوا إِنَّا تَطَيَّرْنَا بِكُمْ لَئِنْ لَمْ تَنْتَهُوا لَنَرْجُمَنَّكُمْ وَلَيَمَسَّنَّكُمْ مِنَّا عَذَابٌ أَلِيمٌ ⑱

18. Wakasema: "Hakika sisi tumekorofika kwa ajili yenu. Kama hamtaacha (kusema haya mnayoyasema ya kutuvuta katika dini yenu) tutakupigeni mawe, na itakufikieni kutoka kwetu adhabu iumizayo."

قَالُوا طَائِرُكُمْ مَعَكُمْ أَئِنْ ذُكِّرْتُمْ بَلْ أَنْتُمْ قَوْمٌ مُسْرِفُونَ ⑲

19. Wakasema: "Ukorofi wenu mnao wenyewe. Oh! Kwa kuwa mnakumbushwa (kheri mnawaambia watu wakorofi?) Ama nyinyi ni watu mnaopindukia mipaka."

وَجَاءَ مِنْ أَقْصَا الْمَدِينَةِ رَجُلٌ يَسْعَىٰ قَالَ يَا قَوْمِ اتَّبِعُوا الْمُرْسَلِينَ ⑳

20. Na akaja mtu mbio kutokea upande wa mbali wa mjini, akasema (kuwambia watu wa mji huu) "Enyi watu wangu! Wafuateni wajumbe (hawa)."

21. "Wafuateni hawa wanaokufundisheni bila ya kutaka ujira; na hali ya kuwa wenyewe wameongoka."

اتَّبِعُوا مَنْ لَّا يَسْـَٔلُكُمْ اَجْرًا وَّهُمْ مُّهْتَدُوْنَ ﴿٢١﴾

22. (Wakamwambia "Kwani wewe umewafuata?" Akasema): "Kwa nini nisimuabudu yule aliyeniumba (na kukuumbeni nyinyi pia) na kwake mtarejeshwa?"

وَمَا لِيَ لَآ اَعْبُدُ الَّذِيْ فَطَرَنِيْ وَاِلَيْهِ
تُرْجَعُوْنَ ﴿٢٢﴾

23. "Je, niishike miungu mengine badala yake? Na kama Mwenyezi Mungu akipenda kunidhuru, uombezi wao hautanifaa kitu, wala hawataniokoa!"

ءَاَتَّخِذُ مِنْ دُوْنِهٖٓ اٰلِهَةً اِنْ يُّرِدْنِ الرَّحْمٰنُ بِضُرٍّ لَّا
تُغْنِ عَنِّيْ شَفَاعَتُهُمْ شَيْـًٔا وَّلَا يُنْقِذُوْنِ ﴿٢٣﴾

24. "Nikifanya hivyo nitakuwamo katika upotofu (upotevu) ulio dhahiri."

اِنِّيْٓ اِذًا لَّفِيْ ضَلٰلٍ مُّبِيْنٍ ﴿٢٤﴾

25. "Bila shaka mimi nimemuamini Mola wenu (huyo ninayekuambieni), basi nisikilizeni, (na nyinyi mumuamini." Hawakusikiliza maneno yake, bali walimuua.)

اِنِّيْٓ اٰمَنْتُ بِرَبِّكُمْ فَاسْمَعُوْنِ ﴿٢٥﴾

26. Akaambiwa "Ingia Peponi." Akasema: "Laiti watu wangu wangejua (haya niliyoyapata wakapata nao kusilimu)"

قِيْلَ ادْخُلِ الْجَنَّةَ ۗ قَالَ يٰلَيْتَ قَوْمِيْ يَعْلَمُوْنَ ﴿٢٦﴾

27. "(Wangejua) jinsi Mola wangu alivyonisamehe na akanijaalia miongoni mwa waliohishimiwa."

بِمَا غَفَرَ لِيْ رَبِّيْ وَجَعَلَنِيْ مِنَ الْمُكْرَمِيْنَ ﴿٢٧﴾

28. Na hatukuwateremshia watu wake jeshi kutoka mbinguni (kuwaangamiza) baada yake; wala hatukuwa wateremshao (majeshi mbinguni kwa ajili ya kuangamiza. Malaika mmoja tu anatosha).

وَمَآ اَنْزَلْنَا عَلٰى قَوْمِهٖ مِنْۢ بَعْدِهٖ مِنْ جُنْدٍ مِّنَ
السَّمَآءِ وَمَا كُنَّا مُنْزِلِيْنَ ﴿٢٨﴾

29. Basi hakukuwa (kuangamizwa kwao) ila kwa ukelele mmoja tu (uliopigwa na Jibrili); na mara wakawa waliozimika, (Waliokufa)!

اِنْ كَانَتْ اِلَّا صَيْحَةً وَّاحِدَةً فَاِذَا هُمْ خٰمِدُوْنَ ﴿٢٩﴾

30. Inafaa kusikitikiwa hawa waja (wa Mwenyezi Mungu): hakuwajia Mtume yoyote ila walikuwa wanamfanyia mzaha (na wanakataa kumfuata)!

يٰحَسْرَةً عَلَى الْعِبَادِ ۚ مَا يَأْتِيْهِمْ مِّنْ رَّسُوْلٍ اِلَّا
كَانُوْا بِهٖ يَسْتَهْزِءُوْنَ ﴿٣٠﴾

31. Je, hawaoni uma ngapi tuliziangamiza kabla yao? (Hawaoni) kuwa hawarejei kwao?

اَلَمْ يَرَوْا كَمْ اَهْلَكْنَا قَبْلَهُمْ مِّنَ الْقُرُوْنِ اَنَّهُمْ اِلَيْهِمْ لَا
يَرْجِعُوْنَ ﴿٣١﴾

32. Na hapana (viumbe) wowote ila watahudhurishwa mbele yetu.

ع وَاِنْ كُلٌّ لَّمَّا جَمِيْعٌ لَّدَيْنَا مُحْضَرُوْنَ ﴿٣٢﴾

33. Na alama (ya kuonyesha moja ya rehema za Mwenyezi Mungu) juu yao ni ardhi iliyokufa: Tunaifufua na tukatoa ndani yake nafaka, wakawa wanazila.

وَاٰيَةٌ لَّهُمُ الْاَرْضُ الْمَيْتَةُ ۚ اَحْيَيْنٰهَا وَاَخْرَجْنَا
مِنْهَا حَبًّا فَمِنْهُ يَأْكُلُوْنَ ﴿٣٣﴾

34. Na tukafanya ndani yake mabustani ya mitende na mizabibu na kupitisha chemchem ndani yake

وَجَعَلْنَا فِيْهَا جَنّٰتٍ مِّنْ نَّخِيْلٍ وَّاَعْنَابٍ وَّفَجَّرْنَا
فِيْهَا مِنَ الْعُيُوْنِ ﴿٣٤﴾

35. Ili wale katika matunda yake; na haikuyafanya (matunda) hayo mikono yao; je, hawashukuru?

لِيَأْكُلُوا مِن ثَمَرِهِ وَمَا عَمِلَتْهُ أَيْدِيهِمْ أَفَلَا يَشْكُرُونَ ٣٥

36. Ametukuka Mwenyezi Mungu aliyeumba dume na jike katika (vitu) vyote; katika vile ivioteshayo ardhi, na katika nafsi zao (wanaadamu), na katika vile wasivyovijua.

سُبْحَانَ الَّذِي خَلَقَ الْأَزْوَاجَ كُلَّهَا مِمَّا تُنبِتُ الْأَرْضُ
وَمِنْ أَنفُسِهِمْ وَمِمَّا لَا يَعْلَمُونَ ٣٦

37. Na usiku ni alama kwao (vile vile ya neema za Mwenyezi Mungu juu ya viumbe vyake); tunauvua humo mchana; mara wao wanakuwa kizani

وَآيَةٌ لَّهُمُ اللَّيْلُ نَسْلَخُ مِنْهُ النَّهَارَ فَإِذَا هُم
مُّظْلِمُونَ ٣٧

38. Na jua (pia ni alama kwao); linakwenda (maisha) mpaka kituoni pake. Hayo ni matengenezo ya (Mwenyezi Mungu) Mwenye nguvu (na) Mwenye kujua.

وَالشَّمْسُ تَجْرِي لِمُسْتَقَرٍّ لَّهَا ذَٰلِكَ تَقْدِيرُ الْعَزِيزِ
الْعَلِيمِ ٣٨

39. Na mwezi (kadhalika ni alama kwao); Tumeupimia vituo, (hiki baada ya hiki); mpaka unakuwa (mwembamba) kama chaparare la mtende kuukuu (lililonywea).

وَالْقَمَرَ قَدَّرْنَاهُ مَنَازِلَ حَتَّىٰ عَادَ كَالْعُرْجُونِ
الْقَدِيمِ ٣٩

40. Haliwi jua kuufikia mwezi, (wakati wa nguvu zake) wala usiku kuupita mchana, (ukaja kwa ghafla kabla ya wakati wake). Na vyote vinaogelea katika njia (zao)

لَا الشَّمْسُ يَنبَغِي لَهَا أَن تُدْرِكَ الْقَمَرَ وَلَا اللَّيْلُ سَابِقُ
النَّهَارِ وَكُلٌّ فِي فَلَكٍ يَسْبَحُونَ ٤٠

41. Na ni alama kwao (vile vile ya kuonyesha neema zetu juu yao) kuwa tuliwachukua wazee wao katika majahazi yaliyoshehenewa

وَآيَةٌ لَّهُمْ أَنَّا حَمَلْنَا ذُرِّيَّتَهُمْ فِي الْفُلْكِ
الْمَشْحُونِ ٤١

42. Na tukawaumbia (viumbe waliokuja baada yao na wanaozidi kuja; tumewaumbia) vipando mfano wa (majahazi, lakini vilivyo vizuri zaidi na vya raha zaidi, kama hizi meli) watakavyovipanda.

وَخَلَقْنَا لَهُم مِّن مِّثْلِهِ مَا يَرْكَبُونَ ٤٢

43. Na kama tukitaka tutawagharikisha (juu ya kuwa vyombo hivi ni madhubuti sana) wala hatakuwako wa kuwasaidia, wala hawataokolewa (maadamu hatutaki)

وَإِن نَّشَأْ نُغْرِقْهُمْ فَلَا صَرِيخَ لَهُمْ وَلَا هُمْ
يُنقَذُونَ ٤٣

44. Ila kwa rehema zitokazo kwetu na kuwanufaisha kwa muda kidogo (tu hivi).

إِلَّا رَحْمَةً مِّنَّا وَمَتَاعًا إِلَىٰ حِينٍ ٤٤

---

36. Ndiyo kwanza sasa watalaamu wa ulimwengu wamejua kuwa kumbe hata katika visivyokuwa na roho kuna madume na majike, na kwa mchanganyiko wao ndipo vinapopatikana vinavyopatikana. Na Qurani imetaja haya zamani, na Mwenyezi Mungu akasema humo katika Aya ya 53 ya *Surat Ha Mym Sajdah*, kuwa "Tutawaonyesha (ukweli wa) maneno yetu katika pande zote za ulimwengu, na katika nafsi zao wenyewe, mpaka iwabainikie kuwa haya (yanayosemwa na Qurani) ndiyo haki." Basi Qurani ndicho kitabu cha haki kisichokuwa na upogo wala kosa hata chembe.

42. Huu ukweli mwingine wa Qurani Kiasi cha miaka alfeni imebashiri kuja meli na manuwari na masabmarini na motaboti na vyinginevyo vya kwenda baharini. Na ikabashiri kwa kuja mareli, (magari ya moshi) na mamotakari na mabaiskeli na mabasi na maaropleni na mengineyo katika Aya ya 8 ya *Suratun Nahl.* Na ikabashiri pia Qurani kwenda mbinguni — kama wanavyojitahidi watu sasa kutaka kufanya. Mahala pamoja katika ilipoyabaini haya ni katika Aya ya 13 ya *Suratul Jaathiya.*